MEI - JUNI MMXXVI - TOLEO LA LII

NGURUMO

ya Mwandishi

DINA TULI ATULIA KWA MUUMBA...

HABARI KUU:

•TUZO NYERERE YA UANDISHI BUNIFU MSIMU WA NNE YATIKISA

Kava: Marehemu Dina Tuli, R.I.P

HADITHI

SINDBAD BAHARIA—Uk 15

K.O.K.W.A—Uk 25 & 26

KIAPO—Uk 27 – 28

DAWATI LA WATOZI

+255 766974865 - WHATSAPP

+255 672 160 016 Piga

Richard Mwambe

YALIYOMO

MWANDISHI WETU
FRANK JAMES SILAA — Uk 3

PITIO LA VITABU
DIWANI: CHUNGU TAMU — Uk 5

SAIKOLOJIA
USICHANGANYWE AKILI — Uk 5 Uk 6

MAKALA
KISWAHILI KIMATAIFA — Uk 7 Uk 8

KUTOKA KWA FANANI
UKIIHESHIMU FASIHI — Uk 9

SAKO KWA BAKO
MERVAT SAKR — Uk 10

KUTANA NA MWANDISHI
JOSEPH SHALUWA — Uk 11 Uk 12

KURUNZI
TUCHAWA — Uk 13

HABARI MOTO
TUZO NYERERE — Uk 16

SHUBAKA LA VITABU
MJUE ABBAS MAHMOOD — Uk 17

KITABU NILICHOSOMA
MY LIFE MY PURPOSE — Uk 18

KUTOKA MAKTABA
DKT. NDYANAO BALISIDYA — Uk 22

ELIMU JAMII
SAFARI YA MALEZI — Uk 23 Uk 24

MWANDISHI WETU

Frank James Silaa

Toleo letu la 52, katika safu ya MWANDISHI WETU tunammulika mwandishi Frank James Silaa. Huyu ni mmoja wa waandishi wanaofanya vizuri katika uandishi wa mitandao ya kijamii. Ni miezi michache tu iliyopita alipochapisha riwaya yake ya GIZA GIZANI. Hebu basi yeye mwenyewe ajieleze kwetu, tumjue...

Jina langu ni FRANK JAMES SILAA, mkazi wa Arusha. Ni mwandishi wa riwaya lakini pia najishughulisha na uandaaji wa maudhui mitandaoni.
Mimi tangu utotoni ni mpenzi wa kusoma vitabu vya aina mbalimbali vikiwemo vya hadithi. Tabia hii nimeirithi kutoka kwa baba yangu, ambaye ni mpenzi wa kusoma vitabu vya aina mbalimbali.

Safari yangu ya uandishi ilianza baada ya kujiunga na chuo kikuu mwaka 2014. Hapo ndipo nilipopata muda wa kuanza kuandika na kupost kwenye mtandao wa facebook. Hadithi yangu ya kwanza kabisa ilikuwa inaitwa NO WAY OUT.

Hii ni hadithi ambayo niliandika kwa hisia sana maana kwa kiasi fulani iligusa historia ya maisha yangu. Ilipata mwitikio mkubwa sana. Ndipo nikapata wazo la kufungua *page* nikaiita Story za Frank.
Baada ya hapo nikaandika riwaya nyingine inaitwa LAITI NINGEJUA. Nashukuru Mungu nayo ilipokelewa vizuri sana. Ikanifungulia milango ya kufahamiana na waandishi mbalimbali kama Emmanuel F Kway (Story za Kway) na Bahati Mfilinge (Mfilinge Stories Tz).

Mungu awabariki sana hawa jamaa maana walitokea kuamini kipaji changu *since day one.* Lakini pia walinipa sapoti ambayo siwezi kuisahau. Lakini kubwa zaidi hata nilipohisi kukata tamaa walinitia moyo.

Basi bwana, riwaya ya tatu ikawa SHEREHE KUZIMU. Nikazidi kung'ara mitandaoni. Nikaanza kuuza vipande vya stori whatsApp. Nikaprint na fulana za Story za Frank nikauza sana pale UDSM.

Hadithi ya nne ikawa TETEMEKO LA PENZI. Hii sikuimaliza kwa sababu ratiba ilinibana sana baada ya kuhitimu chuo.
Nikaingia mtaani. Ule muda wa kuandika nikaukosa. Nikapotea hewani hadi 2018 niliporejea baada ya kutafutwa na Kway.

Hapo ndipo nilibadili jila la page yangu kutoka Story za Frank na kuwa Frank James Silaa. Nikaendeleaa kuposti riwaya pamoja na hadithi fupi kwa muda mfupi kisha nikapotea tena kwa miaka sita. Nikaja kuibuka mwaka 2025 baada ya kuchapa kitabu changu cha GIZA GIZANI.

Namshukuru Mungu hata baada ya kurudi mtandaoni bado mashabiki walinipokea vizuri. Kwa sasa ukurasa wangu wa Facebook unapokea malipo kutokana na kazi nazopandisha. Lakini kubwa lingine ni kwamba nakala ya kitabu cha Giza Gizani kimeisha sokoni.
Yote haya kwangu nayahesabu kama mafanikio makubwa ambayo yametokana na nguvu kubwa ya mashabiki nyuma yangu. Kwa upendo mkubwa na mimi nimewaandalia mashabiki zangu kazi mpya ambayo itatoka hivi karibuni.

Ukweli ni kwamba napenda kuandika kuliko hata kula. Nadhani hii ndio kazi Mungu ameniitia maana naamini naweza kuifanya hata nikiwa vitani.
Kwa kijana mwenye ndoto ya kuwa mwandishi, asikate tamaa. Aendelee kupambana bila kuchoka maana barabara ya mafanikio ya mtu huchongwa na yeye mwenyewe.

Karibu kwenye ukurasa wangu wa Facebook uitwao (Frank James Silaa). Huko utakutana na kazi zangu kwa asilimia mia moja ingawa siuzi soft copy.
Vitabu vyangu vitaendelea kupatikana Posta kwa George, Kinondoni kona ya riwaya, Arusha kimahama, Konzo Bookshop- Mafinga. Morogoro- Nanenane. Dodoma- Nyerere square. Kwa mawasiliano 0687341398.

KITABU KIPYA MJINI

Mwandishi: HASSAN MBONECHE

Baada ya ukimya wa muda mrefu, mwandishi Hassan Mboneche anakuletea ...

MSAMAHA WA RAIS.

Utata wa mfungwa yupi aliyefariki baina ya Dionizi Mfinanga na Lyabang Mwakipesile unaibuka ndani ya Gereza la Kisongo lililopo mkoani Arusha, baada ya kutoka orodha ya wafungwa waliosamehewa makosa yao na mheshimiwa Rais siku ya kusherehekea uhuru wa nchi. Hilo linajitokeza baada ya jina ambalo wafungwa waliamini mtu huyo amefariki kutokea kwenye orodha hiyo.

Sintofahamu hiyo iliyochukuliwa kama siri na viongozi wa ngazi za juu wa gereza inavuka mipaka na kuangukia mikononi mwa Kurugenzi ya Intelijensia ya Taifa (DNI). Kutokana na umuhimu wake, wanaidara, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Opereseheni za Ndani (DIO) Askofu Ponera, wanaingia kazini kwa haraka ili wabaini ukweli na kuchukua hatua.

Je, nini chanzo na hatima ya utata huo?

Ni kwa Tsh 7000 tu unaburudika mpaka herufi ya mwisho.

7000/=



Jikamatie nakala yako katika maeneo yafuatayo:-

DAR ES SALAAM:
Kona ya Riwaya, Kinondoni Morocco—0655428085
Posta Mpya kwa George—0755454152
MAKAMBAKO—APM Bookshop 0762282599
ARUSHA—Nje ya Jengo la Kimahama kwa Ally Said—0757690302
MOSHI—0673056571

PITIO LA VITABU

CHUNGU TAMU - 07

DIWANI YA CHUNGU TAMU

MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI

WACHAPISHAJI: TPH

MWAKA: 1985

Inatoka toleo lililopita…

5. NAFASI YA MWANAMKE PAMOJA NA UHURU WAKE KATIKA JAMII.

Mwandishi amemchora mwanamke katika nafasi mbali mbali kama ifuatavyo;

Mosi,amemchora kama mwanamapinduzi na jasiri.Katika shairi la "Daktari Askari" mwanamke ameoneshwa akifanya kazi za kimapinduzi sawa na zile za mwanamme. Mwanamke anapigana vita ili aikomboe nchi yake.

Pili,mwanamke amechorwa kama mtu mwenye mapenzi ya dhati katika jamii. Katika shairi la "Manzese Mpaka Ostabei" linamwonesha Dorothy akiwa na mapenzi ya dhati kwa Mashaka. Hali kadhalika katika shairi la "Daktari Askari" linamwonesha Eva akionesha mapenzi ya dhati kwa Daktari Adam.

Tatu, mwanamke amechorwa kama kiumbe laghai, asiye mwaminifu hususani katika suala la mapenzi na ndoa. Haya yote tunayaona katika shairi la "Fikra za Waungwana".

Mwisho, mwanamke amechorwa kama mzazi na mlezi katika jamii. Katika shairi la "Manzese mpaka Ostabei", mwanamke amechorwa kama mzazi na mlezi na hii nafasi inawakilishwa na Dorothy ambaye alimzaa mtoto na kumlea baada ya kuolewa na Mashaka.

Kuhusu uhuru wa mwanamke, msanii ameleta mjadala juu ya uhuru wa mwanamke, uhuru wa kuolewa na wanaume wawili kama afanyavyo mwanaume kwa kuoa wake wawili au zaidi.

Katika shairi la "Fikra za Waungwana" mwandishi anasema;

"Mume wangu nakupenda, Josefu amenikuna

Nimekula naye tunda, nampendelea sana,

Ila usifanye inda, mimi ni wako kimwana,

Nitaishi kwa mpango, kwako na kwake Josefu."



www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Msanii anajadili dhamira hii kupitia mhusika Anna. Katika shairi hili, Anna ana mume wake (Nania) lakini kwa upande mwingine anampenda Josefu ambaye ni mume wake wa pili. Anna haoni sababu ya kutokuwa na wanaume wawili.

Msanii anaonesha kuwa uhuru anaoutaka Anna ni wa kuishi au kuwa na wanaume wawili na huo ndio msimamo wa Anna.

Hata baada ya kesi yake kupelekwa mahakamani, Anna alibaki na msimamo huo huo. Hali kadhalika majaji walishindwa kutoa hukumu, kwani hakuna sheria inayozuia mwanamke kuwa na wanaume wengi kama walivyo wanaume ambao huwa na wanawake wengi.

Lakini swali la kujiuliza ni kuwa, je mwanamke ana haki ya kuwa na wanaume wawili katika jamii? Hakuna sheria inayomzuia mwanamke kuwa na wanaume wawili lakini mila na desturi ndiyo zinazomzuia mwanamke kuwa na waume wawili. Hivyo ni kutokana na kasoro hizo ndiyo maana anapinga kasoro hizo, kudai uhuru wake wa kuolewa na wanaume wawili kwa wakati mmoja kama mwanaume anavyooa wake wawili au zaidi kwa wakati mmoja.

Hivyo anaishauri jamii kuona inaweka wazi sharia zinazohusiana na suala hili. Majaji walishindwa kuhukumu kesi ya Nania- hii ni kwasababu hakuna kifungu cha sheria kinachomzuia mwanamke kuolewa na wanaume wawili kwa wakati mmoja.

Itaendelea toleo lijalo

SAIKOLOJIA

Na: NEEMA MGAO

MALKIA WA SAIKOLOJIA

+255763013206

USIRUHUSU KUCHANGANYWA KICHWA/AKILI.

Ni wakati mwingine tena mzuri tunakutana katika safu hii ya saikolojia. Ni matumaini yangu kuwa upo salama kabisa, kimwili na kiakili. Ikiwa kuna mushkeri au utofauti wowote ni maombi yangu kwa Mungu akupe ahueni na uponyaji wa hapo ulipokwama. Ikiwa mambo yanaenda vizuri basi ungana nami kusoma jarida na hasa makala hii ili uweze kujiongezea kama si kupata elimu ya kisaikolojia.

Katika toleo hili na hasa kwenye Makala hii tutazungumzia namna nzuri ya kukataa kuruhusu kuchanganywa kichwa au akili yako.

Utakubaliana na mimi, kama haijawahi kukuta basi uliwahi kusikia watu wakitumia msemo huu, UNANICHANGANYA KICHWA (AKILI YANGU) wakimaanisha kufanyiwa tukio lililoondoa utulivu wa akili yake au amani ya akili yake. Inawezekana kabisa kuwa hata wewe umewahi kufanyiwa tukio ambalo limeondoa uhimili wa akili yako. Unaweza kufanyiwa mambo mengi ambayo yataondoa au yatakuondoa kwenye uimara wa akili yako, tuyaone kwa uchache,.

A]. KUSALITIWA WAZIWAZI.

Mke au mume, mpenzi au mchumba, akiwa anajua kuwa unampenda, anajua kabisa wewe *hupindui* juu yake, kwa makusudi kabisa anaamua kukuonyesha kuwa yupo na mahusiano na mtu mwingine. Aidha ukamfumania na wala asijali wala kuonyesha kujutia kiasi cha kukufanya utamani kumfundisha namna nzuri ya kukuomba msamaha. Ni wazi kuwa atakua ameuondoa uimara wa akili na kukuchanganya kichwa chako.

B]. KUONYESHWA CHUKI YA WAZI

Kila binadamu anaishi kwa kutarajia na kutegemea kupendwa. Hakuna anayeishi huku akitegemea kuonyeshwa au kufanyiwa chuki. Wapo watu kwa makusudi kabisa wataamua kukuonyesha kuwa wanakuchukia. Wakati mwingine watakutamkia wazi wazi kuwa WANAKUCHUKIA. Watu hao wanaweza kuwa ni wale wa karibu sana, pengine watoto, wazazi, mwenzi wako au wale watu ambao wamepitia mikononi mwako, aidha wadogo zako au wakubwa zako. Yote hiyo ni katika kuhakikisha wanaivuruga akili yako ili ujitoe thamani.

C]. KUHARIBIWA MIPANGILIO YAKO

Kila binadamu anaongozwa na mipango yake binafsi, ilimradi yupo na akili timamu basi ni lazima awe na mipango binafsi. Na kwakuwa tunaishi tukitegemeana, yaani hapo ulipo yupo mtu unamtegemea katika kukamilisha mambo yako, unaweza kuwategemea wafanyakazi wenzio hapo ofisini, unaweza ukamtegemea mfanyakazi wako wa ndani, unaweza ukawategemea majirani zako, yaani maisha ni

kutegemeana. Katika kutegemeana unaweza kujikuta matarajio yako yakavurugwa na hao hao unaowategemea. Pengine unamtegemea mfanyakazi wako wa ndani, kwamba wewe ni mama na umetoka kwenye likizo ya uzazi, unarejea kazini na hapo nyumbani unamtegemea dada wa kazi akae na mtoto huyo wa miezi mitatu hadi muda ambao wewe unatoka kazini, ghafra dada wa kazi akatoroka nyumbani, haibi chochote, anasubiri muda ambao wewe huwa unarudi ndipo anaondoka, nakuuliza utachanganyikiwa au utakuwa kawaida?.

Mifano hiyo hapo juu ni baadhi ya matukio ambayo mwanadamu yeyote yule ikimtokea ni lazima achanganyikiwe na kukosa utulivu.

Wapo watu ambao hupata madhara makubwa kisaikolojia, pale ambapo wakutanapo na mambo mazito mfano wa hayo hapo juu. Wengi huingia katika sonona ndogo ambapo ikiwa watachelewa kujiweka sawa hujikuta katika kiwango kikubwa cha sonona kiasi cha kupoteza muhimili wa utimamu wa akili yake. Tuone baadhi ya mambo ambayo yakifanywa huweza kumuokoa mtu asipitie msongo wa mawazo wakati akutanapo na mambo yatakayomchanganya kichwa na akili yake.

POKEA JAMBO

Ni kweli umekutana na jambo gumu na limekuchanganya. Jambo la kwanza kabisa unalopaswa kulifanya ni kulipokea jambo hilo. Pokea na ulikubali kuwa limekufika.

TAFAKARI ATHARI NA MANUFAA YAKE

Kila jambo lina pande mbili, lina ubaya na lina uzuri wake, ukishalipokea jambo lililokutokea basi orodhesha athari hasi na athari chanya. Jua wema na ubaya wa jambo hilo.

PUUZIA

Kwakua lengo ni kukuvuruga kichwa basi ni dhahiri shahiri kuwa jambo hilo ni baya. Ili uwe salama kisaikolojia jifunze kupuuzia matatizo yenye lengo la kukuchanganya ufahamu wako. Hata yawe makubwa kiasi gani, dogosha mambo, yaone kama madogo tuu.

TATUA TATIZO KWA UTULIVU

Baada ya kulipuuzia na kulidogosha tatizo, sasa tatua tatizo husika kwa utulivu kabisa.

SHIRIKISHA UNAEMUAMINI

Katika utatuzi wa mambo yako, usikae kimya, mshirikishe mtu mmoja au wawili unaoamini kuwa wataambatana nawe katika utatuzi wa jambo lako.

Baada ya kupita katika hatua hizo, hongera, wewe ni mshindi katika maisha yako. Ukipita katika hatua hizo, utaona unatatua mambo bila kuhaha, utatatua changamoto kwa utulivu wote.

Ndugu msomaji, kwa huduma za ushauri wa kisaikolojia, kuhusiana na mapenzi, mahusiano, ndoa, malezi ya watoto wako iwe wa kuwazaa au wa kufikia, malezi ya vijana na ushauri kuhusu maisha kwa ujumla karibu uwasiliane nami ili nikushauri na kukuvusha hapo utakapokua umekwama, tumia namba +255763013206 naitwa Madam Neema Mgao, napatikana DODOMA, TANZANIA.

Sambamba na huduma hizo za ushauri pia mimi ni mwandishi wa vitabu vya kisaikolojia, mpaka sasa vipo vitabu vinne vinavyopatikana popote utakapovihitaji, JIJENGE KISAIKOLOJIA, JITIBIE KISAIKOLOJIA, SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA na GABEDA [MWANAMKE WA DHAHABU]. Kupata vitabu hivi wasiliana name kupitia +255763013206 . Nifate kule FACEBOOK kwa jina la NEEMA MGAO ili kupata taarifa namaswala kede kede ya niyafanyayo.

KARIBU SANA.

KISWAHILI KATIKA MAJUKWAA YA DUNIA

Na Mervat Sakr

Kwa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kiswahili… Wakati Lugha Inaandika Historia ya Baadaye

Utangulizi: Sauti ya Bara na Nafsi Yake ya Pamoja

Kila tarehe saba Julai, dunia haiadhimishi tu lugha inayotumika katika mawasiliano ya kila siku, bali husimama mbele ya tukio la kipekee la kiisimu na kitamaduni lililoweza, kwa karne nyingi, kusuka utambulisho wa Afrika katika mfumo mmoja wenye mshikamano. Hii ni lugha ya Kiswahili, ambayo haibaki kuwa chombo cha mawasiliano pekee, bali imekuwa ishara ya umoja, hifadhi ya kumbukumbu ya pamoja, na nyenzo laini ya kuunda upya uwepo wa Afrika katika ulimwengu.

Kupitishwa kwa siku hii na UNESCO kama Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kiswahili ni kilele cha safari ndefu ya athari za kihistoria na kitamaduni, pamoja na utambuzi wa kimataifa wa lugha iliyofanikiwa kuvuka mipaka ya kijiografia na kuwa mojawapo ya lugha zinazoenea zaidi barani Afrika, na pia yenye uwezo mkubwa wa kubadilika na kujijenga upya.

Kama mtafiti wa isimu, sioni Kiswahili kuwa mfumo wa lugha tu, bali nakisoma kama simulizi jumuishi ya ustaarabu; simulizi linalothibitisha kuwa lugha inaweza kuwa chombo cha umoja, si cha utawala, na daraja la kukutana, si njia ya kutenga.

Kwanza: Lugha Isiyo na Mipaka… Jinsi Kiswahili Kilivyoshinda Bila Ukoloni

Tofauti na lugha nyingi zilizoenea kupitia ukoloni au nguvu za kisiasa, Kiswahili kilichukua mkondo wa kipekee; kilienea kupitia biashara, mwingiliano wa kitamaduni, na roho ya uwazi iliyotawala jamii za pwani ya Afrika Mashariki.

Kuanzia bandari za Bahari ya Hindi hadi ndani ya bara, Kiswahili hakikulazimishwa, bali kilichaguliwa. Jamii zilikikubali kwa sababu kilizungumza nao, si kwa sababu kililazimishwa juu yao. Hili linaipa Kiswahili hadhi ya kipekee miongoni mwa lugha za dunia.

Kiswahili kimekabiliana na mawimbi ya athari za lugha kutoka Kiarabu, Kiajemi, Kireno na Kiingereza; hata hivyo, hakikuyeyuka ndani yake, bali kilifanya mchakato wa "kujibadilisha upya" kwa ustadi, uliokiwezesha kuhifadhi muundo wake na utambulisho wake katika mfano adimu wa unyumbufu wa kiisimu unaoambatana na uthabiti wa kitamaduni.

Pili: Kutoka Uenezi wa Kieneo hadi Kimataifa… Kiswahili Katika Majukwaa ya Dunia

Utambuzi wa kimataifa wa Kiswahili haukuwa ishara ya heshima tu, bali ni dalili ya mabadiliko ya kina katika mizania ya uwepo wa kitamaduni duniani. UNESCO ilipotangaza siku ya kimataifa ya lugha hii, ilitambua kwamba Afrika si tena mpokeaji wa maarifa pekee, bali mshiriki katika kuyazalisha na kuyaelekeza.

Leo, zaidi ya watu milioni 200 wanazungumza Kiswahili, jambo linalokifanya kuwa mojawapo ya lugha zinazoenea zaidi barani Afrika, na chenye uwezo mkubwa wa kuwa lugha ya kazi katika taasisi nyingi za kikanda na kimataifa.

Hali hii inaipa Kiswahili nafasi mpya katika diplomasia ya kitamaduni, ambapo lugha inakuwa chombo cha ushawishi na njia ya kuwasilisha Afrika kwa sauti yake yenyewe.

Tatu: Falsafa ya Neno… "Undugu" kama Mfumo wa Maisha

Nguvu ya Kiswahili imo katika kina cha maana zake. Maneno yake hubeba zaidi ya maana ya kamusi; hubeba maadili ya kijamii na kitamaduni.

Neno kama "Undugu" (uhusiano wa kindugu) halirejelei tu uhusiano wa kibaolojia, bali linaakisi mtazamo mpana wa mahusiano ya kibinadamu unaojengwa juu ya mshikamano na hisia ya kuwa na uhusiano wa pamoja. Kutokana na hilo, tunaweza kuelewa jinsi lugha inavyochangia katika kujenga kile kinachojulikana kama "amani chanya", ambayo haijikiti tu katika kukosekana kwa migogoro, bali katika kuimarisha maadili ya kuishi pamoja na kuheshimiana.

Kwa maana hii, Kiswahili si lugha tu, bali ni mfumo wa fikra unaounda upya namna binadamu anavyomwona mwingine, na kuthibitisha kuwa tofauti inaweza kuwa chanzo cha nguvu, si mgawanyiko.

Nne: Watafsiri na Watafiti… Walinzi wa Da-

raja la Lugha

Katika muktadha huu, nafasi ya watafsiri na watafiti inazidi kuwa muhimu. Jukumu lao haliko tena katika kuhamisha maneno kutoka lugha moja hadi nyingine, bali katika "kutafsiri utambulisho."

Mtafsiri wa leo hubeba jukumu la kusafirisha fikra, tamaduni, na muktadha, na kushiriki katika kuunda taswira ya Afrika kimataifa.

Kadiri dunia inavyozidi kuwa ya kidijitali, umuhimu wa kuzalisha maudhui bora kwa Kiswahili unaongezeka, ili kuhakikisha uwepo wa lugha hii katika maarifa ya kisasa, na kuwapa vijana wa Afrika uwezo wa kujieleza kwa lugha yao bila upotoshaji.

Tano: Kuelekea Uhuru wa Lugha wa Afrika… Kiswahili kama Mfano wa Baadaye

Katika dunia yenye ushindani mkubwa wa kitamaduni na kielimu, lugha imekuwa nguzo ya msingi ya uhuru wa kitaifa na wa bara. Kiswahili kinajitokeza kama mfano wa kile kinachowezekana pale lugha za Kiafrika zinapowekezwa kimkakati.

Kiswahili kina uwezo si tu wa matumizi ya mawasiliano, bali pia wa kuzalisha maarifa. Hii inahitaji kukipeleka katika elimu ya juu, utafiti wa kisayansi, na uchumi wa maarifa, ili kiwe chombo cha ubunifu na si upokeaji tu.

Vilevile, kuingizwa kwa Kiswahili katika sera za lugha za kitaifa na kikanda, hasa ndani ya taasisi za Umoja wa Afrika, kunaweza kuchangia kupunguza pengo la lugha linalokwamisha ujumuishaji wa bara, na kuimarisha fursa za kujenga hotuba ya pamoja ya Kiafrika inayoweza kuingiliana na dunia kutoka katika nafasi ya usawa na si utegemezi.

Katika enzi ya uchumi wa kidijitali, Kiswahili kinaweza kuwa lugha muhimu katika teknolojia na akili bandia kupitia uundaji wa maudhui, mifumo ya lugha, na matumizi ya kidijitali. Hivyo, kuwekeza katika Kiswahili ni kuwekeza katika mustakabali wa Afrika.

Zaidi ya hayo, kukuza Kiswahili kunarejesha hadhi ya utambulisho wa Kiafrika na kuwapa vijana imani kuwa lugha zao zinaweza kueleza sayansi, fikra, na ubunifu.

Wito wa "Kujitegemea" (kujitegemea/kujitawaza) hapa unapata mwelekeo wa kina zaidi; hauko tena kama kauli mbiu tu, bali kama mradi wa kistaarabu uliojumuisha, unaoanzia katika lugha na kupanuka hadi uchumi, maarifa na siasa. Kumiliki lugha, kwa msingi wake, ni kumiliki uwezo wa kujitambulisha, kuunda simulizi lako mwenyewe, na kuchora taswira ya mustakabali.

Hivyo basi, Kiswahili hakisimami tu kama chaguo la kiisimu, bali kama dau la kimkakati la kujenga Afrika iliyo huru zaidi, yenye uwepo mkubwa zaidi, na yenye uwezo zaidi wa kuzungumza kwa sauti yake yenyewe… na kuusikilizisha ulimwengu sauti hiyo kwa uwazi na ujasiri.

Hitimisho: Afrika Inapozungumza kwa Sauti Yake

Mwisho, Kiswahili si lugha tu, bali ni mojawapo ya nyenzo muhimu za nguvu laini ya Afrika. Ni lugha inayofafanua upya uhusiano kati ya utamaduni na utambulisho, na kati ya historia na mustakabali.

Katika siku yake ya kimataifa, hatuisherehekei tu, bali tunaigundua upya, na kutambua kwamba diplomasia ya kweli huanza kwa neno, na kwamba lugha zenye nguvu zaidi si zile zinazolazimishwa, bali zile zinazohamasisha.

Leo, Kiswahili si tu lugha ya bara, bali ni mradi wa mustakabali… na sauti ya Afrika pale inapoamua kuzungumza yenyewe.

Kikundi cha kwaya kilichoimba nyimbo za Kiswahili katkiukumbi wa Umoja wa Mataifa Nairobi, 2025 katika maadhimisho ya Siku ya Kiswaahili duniani.

KUTOKA KWA FANANI

Na Salum Makamba

UKIIHESHIMU FASIHI INAKUHESHIMISHA

Moja ya vitu utakavyovisikia na kuviona katika mataifa yaliyoendelea ni namna waandishi wao wa fasihi walivyo wakwasi na mashuhuri. Kiasi ambacho wakitembea hadharani wanafuatwa na kuombwa picha au saini na kadhalika. Na hilo ni moja ya mambo yanayofanya mataifa hayo yawe yameendelea sana.

Fasihi inafungua ubunifu na fikra kwa kiwango cha ajabu kabisa. Mambo ambayo ndiyo roho ya kupiga hatua katika lolote au chochote hapa duniani.

Jijini London, kuna stesheni iitwayo Baker. Ni kituo cha Treni ya Chini ya Ardhi iliyozagaa katika maeneo mengi ya jiji hilo. Nje ya moja ya lango la kuingia ndani ya stesheni hiyo kuna sanamu. Na ndiyo hasa iliyonifanya niandike kichwa kisemacho, "Ukiiheshimu fasihi, inakuheshimisha."

Sanamu la Sherlock Holmes.

Picha: Salum Makamba

Sanamu hiyo (pichani) siyo ya mtu mashuhuri yoyote. Bali ni sanamu ya mhusika aliyeundwa katika kazi za fasihi. Naam. Mhusika wa kazi za fasihi wala si mwandishi. Mhusika wa kubuni tu.

Unaposoma vitabu vya fasihi kuna tabia ya waandishi wa vitabu hivyo kuwaelezea wahusika wao namna walivyo. Kiasi ambacho unaweza kujenga picha kichwani jinsi wahusika hao wanavyoonekana katika uhalisia.

Sasa nchini Uingereza paliwahi kuishi mwandishi anaitwa Sir Arthur Conan Doyle. Huyu mwamba alimuumba mhusika aitwaye Sherlock Holmes. Mpelelezi, Askari Kanzu au unaweza kumwita kachero. Ambaye alikuwa akipata majibu ya matukio magumu mno yaliyoshindikana akishirikiana na rafiki yake aliyekuwa daktari. Kazi hizo zingalipo hadi leo.

Mhusika huyo akawaingia watu kwelikweli. Wakampenda kufa. Kiasi ambacho akawa ni mashuhuri kwelikweli. Na kuna kipindi mwandishi alipoona amezidi sana kuongelewa akaamua kumuua. We! Watu wakamvaa. Wakamwambia usituletee za kuleta. Mrudishe. Unamuuaje yule. Sisi bado tunamtaka. Na hakika alimrudisha na akaendelea kumwandika hadi mauti yalipomfika (mwandishi).

Sasa pamoja na mwandishi kuwa mtu wa maana hadi kuweza kupewa hadhi ya "Sir." Bado mhusika wake ndiye mashuhuri kumzidi yeye.

Mchongaji mmoja alilichonga sanamu la Sherlock Holmes, kisha kuna makumbusho yake, kisha kuna baa zenye jina lake na kumbi za maonesho ya jukwaani zenye jina lake na kuna filamu zake pia. Upo? Vyote hivyo vinakuwa kwa namna ambayo mtu aliyemsoma Sir Doyle akiona moja kati ya vitu hivyo anasema hii baa ndo yenyewe aliyokuwa anapenda kuingia Sherlock, hili koti ndo kama alilokuwa anapenda kulivaa na hiyo ndo kofia yake na kadhalika.

Ukiwa hapo Baker Station utaona watu kwa watu kutoka mataifa tofauti wanavyoshupaa kupata picha na sanamu hilo. Nisiseme huko kwenye makumbusho, nisiseme wanaotafuta vitabu ili wamsome na kumjua baada ya kuliona sanamu tu. Hayo yote yanajaza pesa kwenye hazina ya Uingereza.

Wakati naondoka eneo hilo (baada ya kulipiga picha sanamu hilo. Ili nami nikaongeze fedha kwenye hazina ya Uingereza kwa kwenda kununua juzuu kamili za Sherlock Holmes) nikamkumbuka Willy Gamba.

Nikabaki kujisemea tu, "Asiyejua maana, haambiwi maana." Labda kuna siku nasi tutajua kwamba tukiiheshimisha fasihi nayo itatuheshimisha.

Hawaa, Nagota kwa utuvu, matao na huba

Salum Makamba "Mwanagenzi"

Mshairi Bingwa wa Afrika,

May 15, 2026, London; Uingereza.

SAKO KWA BAKO:

MERVAT SAKR

MARA nyingi katika jarida letu hususan kwenye safu ya Shubaka la Vitabu, mmesoma kuhusu wanafasihi kutoka nchini Misri.

Katika SAKO KWA BAKO leo hii namtambulisha kwa uwazi muandishi na mtayarishaji wa makala zote hizo. Yeye amekuwa mmoja wa watozi tunaowategemea sana katika kuandaa jarida hili. Anaitwa Mervat Sakry, mrembo wa sura, banati kwa haiba yake… Hapa anajieleza:

Mimi ni mtafiti wa shahada ya uzamili katika isimu ya lugha ya Kiswahili, nikifanya kazi kama mtafsiri na mwandishi wa maudhui kwa Kiswahili, nikiwa na machapisho katika majukwaa ya habari nchini Tanzania.

Ninashika nafasi ya Mratibu wa lugha ya Kiswahili katika Jukwaa la Kimataifa la Nasser, ambapo nasimamia mafunzo ya vijana katika tafsiri na uandishi wa habari, pamoja na kuendeleza maudhui ya lugha.

Nimetunukiwa heshima katika Udhamini wa Nasser kwa Uongozi wa Kimataifa, na nilishiriki katika programu ya Aspire ya Chuo Kikuu cha Harvard mwaka 2025.

Kitaaluma, nina uzoefu kama mtafsiri katika tovuti ya Wizara ya Vijana na Michezo ya Misri tangu mwaka 2019, na kama mhariri wa lugha katika jukwaa la "Misr Alaan". Pia nimeshiriki katika mikutano ya kimataifa kuhusu tafsiri na haki za binadamu.

Kwa sasa, ninashiriki katika miradi ya kikanda kama AMEL na programu ya Mabalozi wa IEP, nikiwa na msisitizo katika masuala ya lugha, kupambana na matamshi ya chuki, na matumizi ya akili mnemba katika kuendeleza lugha ya Kiswahili na kuongeza uwepo wake katika mazingira ya kidijitali.

Kwa maelezo yake yeye mwenyewe, Mervat amejipambanua kama msomaji mahiri wa vitabu vya fasihi ya Kiswahili. Alkadhalika, ana mahusiano na Watanzania wengi kama moja ya njia za kujifunza na kudumu Kiswahili na Uswahili.

Pichani: Mervat Sakr, mwanaisimuwa Kiswahili kutoka Misri

KUTANA NA MWANDISHI JOSEPH SHALUWA

KUTANA NA MWANDISHI ni safu mpya katika jarida letu ambayo itakukutanisha na waandishi mahiri, wakongwe wa fani kutoka hapa Tanzania. Lengo kubwa ni kupata nafasi ya kujifunza kutoka kwao. Karibuni tuanze Pamoja.

Leo katika safu yetu tunaye Mkongwe wa kazi hizi, JOSEPH SHALUWA. Najua, kwa wapenzi wa fasihi hili si jina geni. Kalamu yake imefanya kazi na magazeti maarufu ya Global na mengineyo. Lakini Joseph Shakuwa ni nani hasa?

Kwanza tujuze historia Yako ya maisha Kwa ufupi (zile struggling za kutafuta maisha)

Nimezaliwa mwaka 1983 Moshi mjini, mkoani Kilimanjaro, ingawa siyo Mchagga. Naweza kusema ni mzaliwa wa Moshi lakini mwenyeji wa Singida (Mnyiramba). Nimekulia na kupata elimu yangu mjini Moshi kabla ya baadaye mwaka 2005 kuhamia Dar es Salaam. Kabla ya kuhamia Dar, kazi yangu kubwa ilikuwa ni kinyozi. Ni mtaalamu sana wa barber shop. Nilijifunza tangu nipo shuleni na siku za Wikiendi nilikuwa nakwenda kufanya kazi. Hata siku za mwanzo nilipoingia Dar nilianza kufanya kazi salon. Nilifanya kwanza Magomeni Mwembechai, Manzese Tip Top kisha Tandale.

Na vipi kuhusu safari Yako ya uandishi wa hadithi na habari....

Wakati naanza kuandika magazetini, kwangu haikuwa ngumu sana kupata nafasi. Nilianza na Gazeti la Nipashe, Mwananchi, Dimba, Bingwa, Mseto kama mtunzi wa hadithi tu wa kujitegemea.

Nikiwa Magazeti ya Dimba na Bingwa nilijifunza kwa vitendo uandishi wa habari. Kwa sababu nilikuwa na nia, haikuwa ngumu kuelewa kuandika makala na habari za mastaa.

Baadaye mwezi Machi, 2006 nilijaribu bahati gazeti la Mseto. Nikapata ajira yangu ya kwanza pale kama mwandishi wa habari za burudani.

Mwishoni mwa 2006, nilipigiwa simu na Eric Shigongo, akasema nifike ofisini kwake, wakati huo Kariakoo. Hiyo ilikuwa ni baada ya miezi kadhaa kupita baada ya kuonana naye na kumuomba kazi.

Nilipofika, nilikutana na mkataba wa ajira. Nilifanya kazi kama mwandishi kwa miezi mitatu tu, nikateuliwa kuwa mhariri.

Baadaye kidogo niliondoka na kujiunga na gazeti la Leo Tena kwa miezi kadhaa kabla ya baadaye mwaka 2008 kurejea Global kama Mhariri Msaidizi wa Gazeti la Ijumaa. Nilikaa hapo mpaka mwaka 2014, nikaondoka na kwenda kujiajiri mwenyewe. Mwezi Machi, 2015, nikaitwa New Habari (2006) Ltd kama Mhariri wa Burudani wa Gazeti la Mtanzania Jumamosi.

Nilidumu hapo hadi mwezi Disemba 2018, nikarudi tena Global hadi mwaka 2020 nilipoondoka moja kwa moja. Kwa sasa nafanya shughuli zangu binafsi za kutayarisha, kuchapa na kusambaza vitabu.

Wasomaji wangependa kujua changamoto gani umepambana nazo katika safari yako ya uandishi na umezivukaje...

Sijawahi kukutana na changamoto wala vikwazo. Popote nilipopita katika safari yangu ya uandishi nilipokelewa kwa moyo wa upendo. Hilo namshukuru sana Mungu.

Kuna mtu mmoja katika moja ya mtandao wa kijamii aliuambia umma kuwa *'Tanzania hakuna mwandishi wa riwaya anayetegemea uandishi tu kuendeshea maisha yake'* we unasemaje juu ya hilo?

Hajafanya tafiti. Wapo waandishi wengi wanaoishi kwa kutengemea kalamu tu. Miongoni mwao ni mimi. Unajua maisha na mafanikio yana tafsiri pana kulingana na mtu na mtu, lakini mimi naamini kuweza kuendesha maisha yako ya kila siku ni mafanikio.

Wapo waandishi wengi nawajua wanaendesha maisha yao kwa kalamu. Kwa sababu hawajanirihusu sitawataja.

Binafsi, maisha yangu ni jijini Dar es Salaam, sijapanga. Naishi kwangu. Nikiwa jijini mara chache matumia usafiri wa umma, nasomesha watoto, tuna mashamba matatu.

Kazi kuu ni uandishi. Nawezaje kukataa kwamba kalamu yangu ndiyo inayoendesha maisha yangu? Huyo jamaa hakutafiti kabla.

Vipi kuhusu wewe? Je maisha Yako yanategemea uandishi wa hadithi tu?

Kwa zaidi ya asilimia 70 maisha yangu yanategemea uandishi. Nina vimiradi vidogo vya kawaida kama walivyo Watanzania wengi. Lakini kazi yangu kuu ni kuandika.

Hebu tugeukie fasihi Kwa upande wako Bwana Shaluwa… tueleze juu ya kazi zako ulizowahi kuandika; zipi umechapa vitabu na zipi ulichapa tu kwenye magazeti?

Maisha yangu yote nimeishi

nikiandika. Hata wakati nilipokuwa salon, nilikuwa naandika.
Global ni chuo cha vitendo cha uandishi wa habari. Kwa wote waliobahatika kupita pale, kwao uandishi ni burudani wala siyo kazi.

Najivunia sana kutumia muda wangu mwingi zaidi Global katika uandishi wa habari na utunzi wa hadithi. Nimepikwa, nikapikika!
Nilipojiunga na Global Publishers, maisha yangu yakawa ya kuandika kwa asilimia mia moja. Pale nimejijenga na kujifunza hasa kuandika.

Nimeandika zaidi ya hadithi 50, makala zaidi ya 100 lakini vitabu nilivyochapa ni 21.

Na katika hizo kazi (Riwaya) ipi ambayo wewe mwenyewe ukiisoma unasema 'naaam hapa niliandika'?
Nimeandika riwaya nyingi kwakweli, lakini kila nikisoma CHOTARA, huwa naiona mpya kila siku. Lakini cha ajabu mashabiki wangu wengi wamenipa mrejesho zaidi kwenye HILIKI YA TUNU.

Hebu tueleze, ushiriki wa familia yako katika uandishi wako... Maana nasikia waandishi ni watu mpo *bize* mpaka muda na wenzi wenu mnakosa kabisa, imekaaje hii?
Nashukuru sana familia yangu inaniunga mkono. Kwakweli muda wote huwa nakuwa *busy,* hata nikiwa nyumbani. Kuna wakati nasaidiwa kazi hata na watoto wangu. Vijana wangu wawili wana *element* za uandishi - mmoja - mkubwa ameshaanza. Ni MC anayefanya vizuri tu kwa sasa.
Huyu MC anaitwa Kelvin lakini anatumia jina la MC Shade. Anafanya pia kwenye media za mitandaoni. Ni entertainer mzuri sana. Anajua kutangaza hasa. Lakini pia ni mwigizaji. Ana vipaji vingi. Mdogo wake ambaye yupo darasa la saba (Eric) ni mwandishi naye lakini zaidi mwanamuziki. Hawa wamenichukua mimi hasa.

Naweza kuwa na wazo, hawa vijana wangu wakanisaidia kulipanua na kuliboresha hadi inakuwa rahisi zaidi kuliwasilisha katika maandishi. Najivunia.

Nikiitolea mfano Riwaya yako ya "HILIKI YA TUNU" unajisikiaje ndugu wa karibu kama dada au shangazi wakiisoma, hasa kwa yale uliyoandika… unafikiri wanakutafsirije?
HILIKI YA TUNU ni simulizi ya mapenzi, lakini nimeiandika kwa ufundi sana na kutumia maneno ya tafsida. Uandishi wake ni mzuri sana, hauna shida. Inaweza kusomwa hata kwa sauti, lakini ni kweli haifai kusomwa na watoto.

Vijana wengi wanapenda kuwa waandishi.... Waanzie wapi? Wape uzoefu wako.
Uwanja wa uandishi kwa sasa ni mkubwa sana. Mitandao ya kijamii ni uwanja ulio wazi na wa bure kabisa. Wakati sisi tunaanza, tulitumia zaidi Magazeti hasa ya Michezo na udaku, lakini kwa sasa mitandao imechukua nafasi.

Chipukizi waonyeshe vipaji vyao huko. Watatoboa tu.

JOSEPH SHALUWA

Mwandishi wa Riwaya, Mwandishi wa habari, Mhariri wa habari, na Mfanyabishara

Tuzo za Ushairi Chaguo la Wasomaji ni moja ya mambo yaliyobamba sana jukwaa la fasihi haswa katika uande wa ushairi. Vipaji vichanga vilionesha umahiri katika kughani na kuandika mashairi na tenzi zenye hisia kali zenye kuleta mtetemo wa roho. Lakini TUCHAWA ni kitu gani hasa? Na je nini maono ya muasisi? Huyu hapa Daruweshi Mukulu wa Nyika, Mshindi wa kwanza wa ushairi Tuzo Nyerere Msimu wa tatu.hapa

TUCHAWA, ILIPO NA INAPOKWENDA

1. Tueleze TUCHAWA ni Nini hasa na historia yake, bila kusahau wazo lilitoka wapi na wadau mlioanza nao

TUCHAWA Ni ufupisho wa maneno Tuzo ya Ushairi Chaguo la Wasomaji. TUCHAWA ni jukwaa huru na jumuishi lililoanzishwa mwaka 2024 kwa lengo la kutambua, kuthamini na kukuza vipaji vya washairi wa Afrika Mashariki, huku likihimiza ushiriki wa wasomaji kama sehemu muhimu ya safari ya ushairi.

2. Mafanikio ya TUCHAWA katika msimu wa kwanza bila kusahau matatizo na changamoto mlizokutana nazo.

MAFANIKIO

TUCHAWA tumefanikiwa kuwa sehemu ya ukuaji na kufufua ari ya ushindani katika eneo la USHAIRI katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:

Mosi tumefanikiwa kuongeza ushiriki wa wasomaji katika mchakato wa kutambua na kuthamini juhudi za washairi ndani na nje ya mtandao.

Pili tumeweza kuibua vipaji vipya vya ushairi kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na hata nje ya nchi.

Tatu tumefanikiwa kuanzisha na hata kuchochea mijadala chanya kuhusu ubora wa kazi za fasihi katika zama hizi za kidijitali.

Nne tumeweza kujenga mtandao wa kuwaunganisha washairi, wasomaji na wadau mbalimbali wa fasihi.

Tano na mwisho tumefanikiwa kuifikia jamii kwa ukubwa ambapo tumepata mwitikio mkubwa kutoka kwa vijana, jambo linalothibitisha kuwa ushairi bado una nguvu katika kizazi cha sasa, hususan kupitia majukwaa ya kidijitli.

CHANGAMOTO

Changamoto kubwa tunayokabiliana nayo mpaka sasa ni upatikanaji wa wadhamini na rasilimali fedha.

Kuandaa tuzo zenye viwango bora kunahitaji:

Moja yatukio lililovuta hisia za watu katika TUCHAWA 2025 . Jane David Mwanizuwa alipotangazwa mshindi wa Mshairi bora wa kike. Picha kutoka maktaba.

Gharama za maandalizi na uendeshaji,
Zawadi zenye hadhi na thamani kubwa kwa washindi,

Uendelezaji wa majukwaa ya kidijitali,
Utafiti na tathmini ya athari za mradi.
Vitu ambavyo bila uwekezaji wa kimkakati, juhudi hizi zinaweza kukwama au kushindwa kufikia kiwango kinachostahili.

3. **Maandalizi ya TUCHAWA msimu wa pili, Wigo mliopanua katika ushindani, udhamini upoje mwaka huu tofauti na Mwaka jana**

Tumethubutu kupanua ushiriki kitaifa na kikanda na kupata na hata kuandaa mkakati wa uendelevu wa kifedha na kiutendaji.
Tumeongeza vipengele viwili ambavyo havikuwepo msimu wa kwanza ambavyo ni Mshairi bora wa chuo na Mghani bora wa mwaka.
Kuhusu udhamini bado tunaendelea kuwasiliana na wadau mbalimbali ambao tuliwapelekea barua za kuomba udhamini.

4. Ushiriki wa washairi upoje katika msimu huu wa pili?
Muitikio umekuwa ni mkubwa na unaotia moyo sana.
Kwa awamu hii washairi wengi wamejitokeza na wamekuwa sehemu kubwa ya kuupa thamani ushairi.

5. Kama Mwanzilishi au muasisi unaona mbele kupitia TUCHAWA

Mustakabali wa TUCHAWA ni mzuri kwa sababu kila msimu tumekuwa tukipiga hatua kubwa zaidi kulingana na muitikio wa washairi wenyewe, mapokeo ya wasomaji na ongezeko la mahitaji katika maandalizi.

BURIANI HINDU NUHU

WATUMIAJI wengi wa mitandao, wapenzi wa usomaji wa vitabuna waandishi walijikuta wakipigwa na butwaa na kubaki kimya pasi na neon lolote. Haikuwa rahisi kuamini wala kukubali kuwa Bi. Hindu ametutoka. Mwenyezi-unguampunguzie adhabu ya kaburi.

Taarifa isiyo rasmi inasema kuwa marehemu alishikwa na pumu jioni ya Mei 15 na ndiyo iliyosababisha mauti yake.

Marehemu Hindu alizikwa katika makaburi ya Makanyagio yaliyopo Frelimo mjini Iringa. Mamia ya watu walijitokeza kumsindikiza katika safari yake hiyo ya mwisho. Katika maneno yake ya mwisho kabla ya kuondoka makaburini hapo, kiongozi wa dini aliyekuwa akiongoza maziko yale alimtaja marehemu kama mtu aliyekuwa na msaada mkubwa kwa jamii. Aida alisema wazi kuwa kwa kusoma-comment za watu mtandaoni aligundua kuwa Hindu alikuwa mtu wa watu, aliyetoa sadaka kila ilipohitajika.

Wakili na Mwandishi Mariam Mbano anamuelezea Hindu kama mmoja wa watu wake muhimu katika kundi lake la Marmz Relationship Hub ambalo hutoa misaada mbalimbali katika maeneo anuai ya wahitaji hapa Tanzania. Imesemwa kuwa ni siku hiyohiyo Marehemu alitoa sadaka yake kwa wahitaji na jioni yake Mungu akamchukua.
Ni wema gani aliokuwa nao? Mwenyezi Mungu ampokee Mbinguni.

Ya Kale Ni Dhahabu

SAFARI 7 ZA SINBAD BAHARIA - 02

Maandalizi yalikamilika kwa siku mbili na nikawa nasubiria safari tu. Wiki ilipofika tukaanza safari kwa amani lakini siku ya tatu kabla ya kuingia kisiwa cha kwanza kufanya biashara hali ya hewe ikabadiliki ghafla.

Nikiwa na woga sana juu ya roho yangu nikabaki namuomba msamaha mwenyezi Mungu. Jahazi lilikwenda ovyo ovyo kwa muda wa masaa sita. Manahodha walifanya wawezapo hata wakaamua sasa kuachia hatima kwa Mwenyezi Mungu. Abiria tulianza kutapika na mimi nikiwa mmoja wapo. Kwamuda kadhaa nilipotelewa na kumbukumbu na sikufahamu zaidi. Nilikuja kupata fahamu chombo kilianza kutulia mbele yetu kukiwa na weupe kwa mbali. .

Nilikaa vizuri nipate lujua kinachoendelea. Manahodha walituambia kuwa kwa sasa tunaingia kisiwa cha roc. Kisiwa hiki hakuna wakazi na wanyama pia hakuna au ni wachache. Kuna hadithi ya zamani sana walokuwa wakisimulia mababu kuwa kuna roc aliyekuwa akila mali za watu kama mifugo na kujeruhi wakazi. Hivyo watu wamehama kisiwa hiki. Ni miaka mingi sasa na ni mababu tu wanasimulia hadithi hii. Huenda ni ngano tuu au ni kweli. Hivyo tutaingia hapa kwa ajili ya kupumzika kidogo na kuangalia kama tutapata maji maana safari ni ndefu. Basi tukaingia kisiwani pale na kuanza kuranda randa. Kwakuwa nilitapika sana sikuwa na nguvu za kutosha hivyo nikaelekea kwenye kivuli kikubwa na kujilaza. Nililala sana na nilipokuja kuamka sikuona watu wala jahazi. Kumbe nilisha kimbiwa, niliogopa sana na nisijue nitatokaje pale kisiwani ambapo hakuna watu wala chakula. Nilianza kujuta kwa kukubali kuja. Nilijua sasa hapa kisiwani nitakufa pekeangu kwa kukosa chakula.

Nilianza kukizunguka kisiwa chote kujua nini nitafanya. Jua nalo lilikuwa likizama. Katika kuzunguka nikaona kuna kitu cheupe kwa mbali. Nikaanza kukifata taratibu na nikakuta kama limpira kubwa sana na laiiini. Kuangalia vizuri sikufahamu nini kitu kile. Ghafla nikaona anga inafunikwa na kuna kivuli kikubwa kinaingia nilikimbia kwenda kujificha. Kumbe alikuwa ni ndege roc mkubwa sana yaani mguu wake mmoja ni kama shina la mti. Kumbe lile dude kubwa jeupe ni yai lake.

Basi kiza kilipoingia nilikwenda karibu na ndege yule nikavua kanzu yangu na kufifunga vizuri kwenye miguu ya yule ndege. Niliamini kuwa akiruka atanibeba na kunitoa kwenye kisiwa kile. Basi nilifanya hivyo na kuendelea na imani yangu hiyo. Mambo yakawa kama nilivyotaka asubhi ndege yule aliruka na kunibeba, kwa kuwa sikuwa mzito sana hakujua kama amebeba kitu lamda alijua ni guo tu.

KUELEKEA BONDE LA UOKOZI

Alinibeba akapaa angani sana hata sikuona ardhi. Alikwenda kwa muda wa dakika 30-50 na akatua kwenye bonde lenye milima. Alipotua nikajifungua na kwawoga alishituka na kuniacha pale. Nikaondoka kwa haraka na kujificha asijeniona. Muda haukupita roc alikamata nyoka mkubwa sana na kumkata vipande. Alimla na kuondoka na kipande. Alipoondoka na mimi nikatoka mafichoni pale na kuanza kuchunguza eneo lile na kujua vipi nitatoka pale.

Nilipochunguza zaidi eneo lile nikagungua ni bonde lililopochini sana na limezungukwa na milima mirefu yenye mawe. Ni bonde ambalo katu mtu asingeweza kutoka. Mchana mzima nilikuwa nikitafuta pa kutokea lakini bila mafanikio. Japo nilikuwa najishauri kuwa bora hapa kuliko kule kisiwani. Usiku ulipoingia nilijificha kwenye mapango na kulala. Usingizi haukuja kabisa kwa woga. Kwani uksiku nyoka walokuwa wakiogopa mchana kuliwa na roc walikuwa wakitoka kutafuta chakula.

Muda wote nilikuwa nikimuomba Mungu dua aniokoe na wadudu wabaya usiku ule. Mwenyezi Mungu alinilinda na ulipofika asubuhi nikaendelea na uchunguzi wangu wa eneo lile. Kwa ghafla nilishituliwa na kishindo nyuma yangu. Nilipogeuka nikakuta ni kipande kikubwa cha nyama. Nyama. Hapa nikakumbuka hadithi ya zamani sana juu ya bonde la wawinda madini. Wazee wetu walikuwa wakitusimulia kuwa kuna watu wanawinda madini kwa kutumia nyama. Yaani wanatupa nyama kwenye bonde lenye madini, kisha nyama ile inaganda vipande vya madini na pindi ndege wanapokuja kuchukua nyama ile ambayo ina madini yaloganda kutoka bondeni huwakimbiza ndege wale na wanapoidondosha wanachukua madini.

Pale nikawa nawaza huende hii ikawa ndio njia pekee ya mimi kutoka pale. Nikawa naangalia kama nitaona mtu lakini sikuweza kuona kwani juu ni mbali sana. Basi nikaamza kuokota madini mapande makubwa makubwa. Eneo lile lilikuwa na madini mengi na makubwa yalokuwa waziwazi. Niliokota almasi na dhahabu kwa wingi pamoja na madini mengine.

ITAENDELEA...

Na Mwandishi wetu.

KATIKA miaka hii minne, kumbukizi ya kuzaliwa Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere imekuwa ikiadhimishwa kwa namna yake na wanafasihi wa Tanzania. Tuzo Nyerere ya Uandishi Bunifu inayofanyika kilele kila tarehe 13 ya mwezi wa Aprili kwa miaka minne mfululizo imekuwa kutano kubwa la wanafasihi nchini, majagina kwa wachanga kupitia shindano kubwa la uandishi bunifu Tanzania.

Katika msimu huu wa nne, mgeni rasmi, mwandishi nguli, Abdilatif Abdallah alikabidhi tuzo za washindi wa kwanza katika tanzu ya Riwaya, Ushairi, Tamthiliya na Hadithi za watoto kwa Bishop John Hiluka kutoka Mkoa wa Dar es salaam aliyeashinda kwa riwaya yake ya Waraka Kutoka Gerezani, Abdallah Salim Ngereza kutoka Tanga aliyeshinda kwa diwani yake ya Kiwinda Elimu, Amina Abdulrahman kutoka Zanzibar aliyeshinda kwa hadithi zake za watoto Shumi na Vitungule na Hamis Hussein Kibali aliyeshinda kwa tamthiliya ya Ufalme wa Mabadiliko. Kila mmoja kati ya hawa alijinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzania 10,000,000 pamoja na cheti cha heshima na tuzo ya kupendeza.

Washindi wengine katika nafasi ya pili walikuwa ni Halfan upande wa riwaya, Kombo Abdalah Omar upande wa ushairi, Godlove Kabati Selestine upande wa hadithi za watoto na Elizabeth Godwin Mahenge katika tanzu ya tamthiliya. Washindi hawa wa pili walijinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzania 7,000,000 na cheti cha heshima.

Sambamba na wao walikuwapo pia katika nafasi ya tatu Enock Abiud Maregesi katika riwaya, Hafidhi Ally Makame katika ushairi, Fatuma Salim Suleiman katika hadithi za watoto na Esther Evarist Nyawale katika tamthiliya. Wote hawa wamejinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzania 5,000,000.

Katika msimu huu wa nne hadhira imeshuhudia mabadiliko kadhaa yaliyoongeza ufanisi katika maadhimisho hayo ikiwapo muda, kupunguza hotuba zisizo na mantiki ya kituzo na kadhalika.

Katika hotuba yake mgeni rasmi Mwalimu Abdilatif Abdalla amesema uandishi bunifu haupaswi kuchukuliwa kama anasa, bali ni nyenzo muhimu ya kujenga fikra, kuielewa jamii na kuibadilisha. Pia alisisitiza kuwa ubunifu wa lugha iwe maandishi au masimulizi una jukumu kubwa la kuelimisha, kuibua tafakuri na kuchochea maendeleo ya kijamii.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Mipango na uwekezaji Prof. Kitila Mkumbo alionya kuwa utamaduni wa kutambua na kutuza unakabiliwa na changamoto kubwa katika zama za mitandao ya kijamii. Kwa mujibu huo ni wajibu wa Watanzania kuunga mkono juhudi hizi ili kuendeleza maadili na utamaduni wa kitaifa.

Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu imechukua umaarufu mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na kwa walumbi wote wa Kiswahili duniani. Serikali imetenga kiasi cha Tsh Bilioni 4.2 kwa kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa tuzo hii.

TUZO NYERERE MSIMU WA NNE
'Uandishi bunifu si anasa'

SHUBAKA LA VITABU

Mervat Sakr, mwanaisimu kutoka Misri anaendelea kutuletea simulizi za wanafasihi mbalimbali wa Misri wa enzi na enzi. Ni simulizi za kuvutia zenye kutia mshawasha katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni moja ya zawadi kubwa kwetu Ngurumo ya Mwandishi na kwako msomaji… leo anamleta kwetu Abbas Mahmoud Al-Aqqad

Abbas Mahmoud Al-Aqqad… Wasifu wa akili huru iliyojijengea utukufu kwa kalamu

Abbas Mahmoud Al-Aqqad hakuwa mwandishi wa kawaida katika historia ya utamaduni wa Kiarabu, bali alikuwa ni tukio la kipekee la kielimu na kifalsafa lililofikia hadhi ya vilele vigumu kufikiwa au kufananishwa. Ndani yake aliunganisha vipawa vingi ambavyo ni nadra kukutana katika mtu mmoja; alikuwa mwandishi mahiri, mshairi mbunifu, mkosoaji mwenye maono, mwanahistoria makini, na mwanafikra huru ambaye hakunyenyekea isipokuwa kwa misingi yake binafsi. Yeyote aliyekaribia uzoefu wake alimuona kama bahari pana isiyopimika kina chake, au kama kilele cha juu kisichofikiwa ila kwa juhudi kubwa na msingi mpana wa maarifa na bidii.

Al-Aqqad alizaliwa huko Aswan mwaka 1889, na alikulia katika mazingira rahisi lakini yaliyosheheni maadili ya elimu na maarifa. Licha ya kutomaliza zaidi ya elimu ya msingi, hilo halikuwa kikwazo kwake, bali lilikuwa msukumo wa kujijenga kwa juhudi zake binafsi. Alijitosa katika kusoma kwa shauku kubwa, akajifungulia milango ya fasihi ya Kiarabu na fasihi za dunia, na kuanza kujenga utamaduni wake juu ya misingi thabiti ya ujuzi mpana na tafakuri ya kina. Mikutano ya kielimu aliyohudhuria pamoja na baba yake ilichangia sana katika kuunda ufahamu wake wa mapema, ambapo alifahamiana na vitabu vya turathi na hazina za fasihi, jambo lililowasha ndani yake mwanga wa shauku uliodumu maisha yake yote.



Abbas Mahmoud Al—Aqqad

Katika ajira ya serikali hakupata kile kilichokidhi matarajio yake, hivyo haraka akachoshwa na vikwazo vyake na kuasi dhidi yake akitafuta upeo mpana zaidi. Uandishi wa habari ulikuwa ni uwanja aliouchagua kujieleza na kuifanya kalamu kuwa silaha, fikra na ujumbe. Alianza safari yake ya uandishi pamoja na Muhammad Farid Wajdi, kisha akahama kati ya magazeti mbalimbali hadi akawa miongoni mwa waandishi mashuhuri katika magazeti makubwa kama "Al-Ahram" na "Al-Balagh". Maandishi yake hayakuwa makala za kupita tu, bali yalikuwa misimamo ya wazi ya kifalsafa iliyotetea uhuru, kupinga udikteta, na kuthibitisha haki ya mataifa katika uhuru na heshima.

Alijihusisha pia na harakati za kitaifa, akahusishwa na chama cha Wafd, akitetea misingi yake pamoja na kiongozi wake Saad Zaghloul. Alipambana katika mijadala mikali ya kisiasa na kielimu dhidi ya wapinzani wake. Ujasiri wake ulidhihirika wazi alipokabiliana na mamlaka katika enzi ya King Fuad I, akipinga kuvunjwa kwa katiba, msimamo uliompelekea kufungwa gerezani. Hata hivyo, gereza halikuvunja azma yake, bali lilimzidishia msimamo wa kushikilia kanuni zake, akithibitisha kwamba uhuru wa fikra kwake haukuwa kauli tu bali ni dhamira anayolipia gharama yake bila kusita.

Baada ya kupungua kwa shughuli zake za kisiasa, Al-Aqqad alijitosa kikamilifu katika uzalishaji wa fikra, akafungua upeo mpana wa uandishi na kuacha urithi wa zaidi ya vitabu mia moja pamoja na maelfu ya makala. Aliandika katika nyanja mbalimbali kama fasihi, ukosoaji, historia, siasa na fikra za Kiislamu. Na katika kila uwanja alitoa maono ya kina yanayoonyesha uwezo mkubwa wa uchambuzi na kuunganisha hoja. Miongoni mwa kazi zake maarufu ni mfululizo wa "Al-'Abqariyat", ulioshughulikia haiba za Kiislamu kwa mtazamo wa kisaikolojia na kifalsafa, mbali na simulizi za kawaida, ukizingatia kiini cha binadamu na motisha zake.

Al-Aqqad alijulikana kwa utamaduni mpana usio wa kawaida; hakujifungia katika taaluma moja, bali alisoma katika nyanja mbalimbali kuanzia falsafa hadi sayansi asilia, akiamini kwamba maarifa ni kitu kimoja kisichogawanyika.

Inaendelea ukurasa wa 24

KITABU NILICHOSOMA

MY LIFE, MY PURPOSE – 05

UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA

"MY LIFE, MY PURPOSE"

Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA

{Imetolewa kutoka mtandaoni}



Kati ya mageuzi tuliyofanya yaliyokuwa na utata sana ni kubinafsisha mashirika ya Umma, mageuzi/maboresho ya utumishi, na uuzaji wa nyumba za Serikali.
Kwa kweli mashirika ya Umma yalikuwa yanaendeshwa kwa hasara. Kuna wanaodai kuwa Mwalimu hakkupenda ubinafsishwaji na alisema hivyo hasa wakati wa mtangulizi wake. Mheshimiwa Mkapa anabaini kuwa, lakini Mwalimu hakunisema ana sijui kwa nini, ukweli ni kwamba Mwalimu alikuwa pragmatist na aliona hali halisi. Kwa bahati mbaya sikufuatilia utendaji wa mashirika Mheshimiwa Mkapa anaendelea mashirika tuliyo yaabinafsisha kama ambaavyo nilivyofanya kwa *Regulatory Agencies.*
Pia kweli kuwa tulibinafsisha kwa watu wan je kuliko wazawa.

Pamoja na ugumu na utata wa baadhi ya mageuzi kura zake katika uchaguzi wa mwaka 2000 zilionge zeka kwa asilimia 100%. Hii kwake ilikuwa kuambiwa "Songa mbele, endelea" Na niliendelea, anasema.

Mheshimiwa Mkapa anasimulia kuwa maono yake: ni maisha ya hali ya juu, amani, utulivu na umoja, utawala bora,jamii iliyoelimika na uchumi shindani wenye uwezo wa kukua kiendelevu na mgawanyo shirikishi wa kipato. Ili kuyapata hayo ikaanzishwa *Vision* 2025MKUKUTAMKURABITA *Mini Tiger Plan* 2020TASAF. Wengi katika Baraza la Mawaziri, kwenye Chama na Serikali hawakuviunga mkono. Lakini sasa naiona TASAF kama "High Point" ya Urais wangu, anasema Mheshimiwa Mkapa.Bima ya TaifaMageuzi katika Elimu, DEDP na SEDPMradi wa maji ziwa Victoria.

Kuhusu mahusiano ya ndani na nje, Mheshimiwa Mkapa anabaini kuwa uhusiano katika ya Bara na Zanzibar ulikuwa mgumu na tete lakini alifanikwa kutatua matatizo.
Anasema alikuwa na wasiwasi pale Rais wa Zanzibar Salmin Amour alipotaka kubadilisha sheria na kutawala kipindi cha tatu. Lakini baadae yeye na wafuasi wake wakaamua yaishe. Zanzibar ilianza kupeperusha bendera yake.

Vifo vya watu 22 huko Pemba Januari 2001 vilinishtua na kumhuzunisha sana. Anasema "hili litaendelea kuwa doa katika Urais wangu ingawa sikuwepo lilipotokea".
Anabaini kuwa wakati wa utawala wake, wanadiplomasia walionyesha upendeleo kwa vyama vya upinzani na kukutana nao mara kwa mara, Pia wapo walioamini walistahili upendeleo kuliko wengine.
Kwa upande wa vyombo vya habari ilibidi azoee kukosolewa, kwani waliamini alikuwa *dictator* ingawa alikuwa anashikilia msimamo. Anabaini kuwa alihitaji kuuza sera zake, kwa hiyo akaanzisha utaratibu wa kulihutubia Taifa kila mwezi lakini mhimili mkuu wa kupokea na kutoa mawazo na habari ilikuwa Chama chake CCM na vikao vyake mbalimbali.

Mheshimiwa Mkapa anakiri kuwa, Kabla hajawa Rais, hakujua kuwa kazi moja wapo ya Rais ni kutoa pole. Moja wapo ya mapungufu yangu ni kwamba si mwepesi wa kuonyesha hisia zangu. Mrithi wangu Rais kikwete ni mzuri sana katika hili. "Anasema Mheshimiwa Mkapa.
Mwaka 1996 mafuriko yalisababisha maafa makubwa katika Nchi. Kuzama kwa Mv bukoba kulistua na kuhuwisha sana majanga mengine mengi. Niliwahurumia wafungwa wote waliostahili kunyongwa mpaka kufa.
Anasema ingawa hakatai kukosolewa kisiasa au kisera, kukosolewa binafsi kuliumiza sana. Kwa mfano madai kwamba alimpendelea Baba mkwe wa mwanae katika kubinafsisha mgodi wa makaa ya mawe wa kiwira yalimuumiza sana.

Pia madai kuwa aliwapendelea NET GROUP solutions ltd wakati wa kubinafisha TANESCO kwa sababu ya shemeji yake kulimuumiza sana pia jambo moja lilojitokeza baada ya muheshimiwa kumaliza muda wake ni la *External payment account (EPA).* Mheshimiwa anaeleza kuwa, anavyoelewa urais wake haukuwa wa kwanza kuruhusu ununuzi wa madeni kama huo. Anasema kwanza alisita ila Gavana wa Benki Kuu Daud Bilali alimuelewesha na akasema watakao nunua hayo madeni walikuwa tayari kuchangia mfuko wa kampeni za uchaguzi wa CCM. Wahuni walitumia uaminifu wake kwa chama kumshawishi akubali. "Ninajisikia kuwa nilitumika na kusalitiwa. Na ukweli ni kwamba mimi binafsi sikufaidika na sikupata chochote". Anasema Mheshimiwa Mkapa.
Itaendelea...

HABARI PICHA

Matukio ya wanafasihi

Mwanamuziki Mwanaharakati Vitali Maembe katika meza ya vitabu ya Mkuki na Nyota.

Kalam Salam, kila Alhamis ya kwanza ya mwezi, tukio linalowakutanisha wapenzi wa fasihi; waandishi kwa wasomaji katika ukumbi wa Alliance Francaise. Je umewahi kuhudhuria?

Pichani, Mwalimu Abdilatif Abdalla aliyekuwa mgeni rasmi katika Tuzo Nyerere msimu wa nne akiendesha mjadala katika mkutano wa pembeni uliofanyika tarehe 13 April, 2026

Katika mstari wa mbele, nguli wa kalamu Shaffi Adam Shaffi akiwa pamoja na washiriki wengine kufuatilia mjadala katika Tuzo Nyerere



MALENGA WA KILEO

SIMANZI

Duniani tunapita, kwa Baba tunarejea
Si Mwamedi wala Pita, sote tutaelekea
Kifo hupimi kwa mita, kwamba huku takwepea
Simanzi twasimanzika, sote ni wa Maulana

Tmekopeshwa uhai, pumzi kama zawadi
Tuishi tungali hai, miaka ina idadi
Ukifa nani tadai, hukutimiza ahadi
Simanzi twasimanzika, sote ni wa Maulana

Zilitufika habari, za mtima mbaya kwani
Tukaacha kuvinjari, tusikie kuna nini
Kumbe Mola kamtadari, Tuli wa Kigamboni
Simanzi twasimanzika, sote ni wa Maulana

Dada Tuli katulia, na Muumba kamrudia
Akatuacha twalia, sintofahamu kubakia
Swali 'kajiulizia, yampasani mautia
Simanzi twasimanzika, Sote ni wa maulana

Hadithi metuachia, dada mzuri Tulia
Hamu metubakia, sote twabaki kulia
Simulizi ulosimulia, nani wa kumalizia
Simanzi twasimanzika, Sote ni wa Maulana

Twabaki pekuapekua, hatujui la kufanya
Mola amekuchukua, sisi akatutawanya
Mawazoni mwetu pia, tukabaki tu kusonya
Simanzi twasimanzika, sote ni wa Maulana

Pumzika kwa amani, mikononi pa Manani
Uloishi duniani, yanatosha kukosani
Twakuombea buriani, wetu mzuri fanani
Simanzi twasimanzika, sote ni wa Maulana.

Raha ya Milele umpe ee Bwana na Mwanga wa milele umuangazie…

… Marehemu apumzike kwa amani…. Amina

TAHARIRI

Salaam kwenu nyote!

Leo tunakuleteeni chapisho la 52, safari bado inaendelea. Jambo zuri ambalo tunapenda kuwaeleza ni kuwa, kuanzia mwaka huu 2026, jarida letu litatoka mara sita kwa mwaka. Na katika mwaka huu tutafanya maboresho ya kimuonekano na ikiwezekana kufanya jambo jipya ambalo tutaliweka wazi kwenu siku za usoni.

Toleo letu la 52, linakujia na habari mbili za kusikitisha sana. Hizi si zinginee bali za vifo vya fanani na hadhira. Mwezi uliopita tulipokea taarifa ya kifo cha mwandishi (fanani) aliyejulikana kwa jina la Tuli. Tuli alikuwa mwandishi wa makala na haditi katika mitandao ya kijamii. Akiwa bado anaiburudisha na kuifunza jamii, *dada* mauti alimfika ghafla, naye hakuwa na budi kusema ndiyo. Tunamuombea sana kwa Muumba wake ili amsamehe makosa yake na afurahi naye mbinguni.

Kabla hatujapoa kwa msiba huo, siku za katikati za Mwezi wa Mei hadhira nayo ikafiliwa na msomaji mahiri wa vitabu hususani vya riwaya. Hindu Nuhu, msomaji wa vitabu kutoka Iringa, alitutoka ghafla bin vuuu! Hakuna aliyeamini kati yetu, lakini Waswahili twasema 'Kazi ya Mungu haina makosa'.

Vifo hivi viwili vya ghafla, vyatufundisha nini mimi na wewe ambao bado tunapiga mark-time hapa duniani?

Tupendane, kwa maana upendo hutoka kwa Mungu. Nasi pia siku ya mwisho tutarudi kwake.

Atuwaombee ndugu zetu, lakini nasi tusichoke kutenda mema.

Wakatabahu!

R.R. Mwambe
20 Mei, 2026

KITABU MARKET—Bookshop

www.kitabumarket.co.tz

KUTOKA MAKTABA
DKT. NDYANAO BALISIDYA

Dkt. Ndyanao Balisidya (anayejulikana pia kama May Lenna Balisidya Matteru, 1947–1987) ni miongoni mwa nguzo na tunu muhimu sana katika historia ya fasihi ya Kiswahili na lugha kwa ujumla nchini Tanzania.

NDYANAO BALISIDYA

1947—1987

Kwanini mwanamama huyuakumbukwe na ulimwengu wa wasomi na wapenzi wa Kiswahili Sanifu?

1. Mchango Wake Katika Fasihi (Riwaya na Tamthilia) Yeye ni mtunzi wa kazi mashuhuri zilizowahi kutumiwa sana katika mitaala ya elimu ya sekondari nchini Tanzania:

Riwaya ya Shida (1975): Hii ndiyo kazi yake maarufu zaidi. Riwaya hii inagusia maisha ya kijamii, matatizo ya vijana, na changamoto za kuhama kutoka vijijini kwenda mijini (kama Dar es Salaam) kutafuta maisha, jambo ambalo liliacha funzo kubwa kwa jamii.

Tamthilia ya Ayubu: Kazi nyingine ya jukwaani inayoonesha umahiri wake katika uchambuzi wa mambo ya kijamii na kifasihi.

2. Taaluma na Uongozi wa Kikazi

Mhadhiri UDSM: Alikuwa mhadhiri katika Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kati ya mwaka 1977 na 1987, ambapo alichangia kwa kiasi kikubwa kulea kizazi cha wasomi wa lugha hiyo.

Uongozi BAKITA: Mwaka 1971, alichaguliwa kujiunga na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na alihudumu kama Makamu Mwenyekiti wa baraza hilo kwa mihula miwili, akipigania ukuzaji na usanifishaji wa lugha.

3. Elimu ya Juu na Mapambano ya Kitaaluma Alikuwa mwanamke wa mfano katika zama zake:

Alipata Shahada ya Sanaa (B.A.) UDSM mwaka 1970.

Alipata Shahada ya Uzamili (M.A.) ya Fasihi Simulizi UDSM mwaka 1978.

Alihitimu Shahada ya Uzamivu (Ph.D.) ya Fasihi za Kiafrika kutoka Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison nchini Marekani mnamo Novemba 1987, ikiwa ni miezi michache tu kabla ya kifo chake cha mapema kilichotokea Desemba 1987.

Uhusiano wa Kifamilia: Dkt. Ndyanao alikuwa dada wa mwanamuziki nguli wa zamani wa Tanzania, Patrick Balisidya (aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Afro 70), ambaye hata aliwahi kumtungia wimbo maalum wa harusi miaka ya 1970.

FALSAFA YA UANDISHI WAKE

Falsafa ya uandishi ya Dkt. Ndyanao Balisidya inajidhihirisha kama Uhalisia wa Kijamii (Social Realism) uliohuishwa na Utanzania na Utu (Humanism). Kama mwandishi aliyeibuka katika muongo wa kwanza baada ya Azimio la Arusha (1967), Balisidya hakuvutiwa na uandishi wa kufikirika au wa kufikiria mambo ya mbali; badala yake, kalamu yake ililenga kuwa kioo halisi kinachoakisi jamii ya Kitanzania—matatizo yake, mabadiliko yake, na matumaini yake.

Tunaweza kuigawa falsafa ya uandishi wake katika misingi mikuu minne:

1. Falsafa ya "Ukweli Mchungu" (Social Realism)

Balisidya aliamini kuwa fasihi inapaswa kusema ukweli bila kuupamba. Katika riwaya yake ya Shida, anaonesha mgongano mkubwa kati ya maisha ya kijiji na mji (Dar es Salaam). Falsafa yake hapa ni kwamba 'maendeleo ya kweli ya binadamu yanajengwa kwa kufanya kazi kwa bidii mahali alipo' na sio kukimbilia mijini kunakochochewa na ndoto za uongo. Haogopi kuonesha upande wa giza wa mji—upotevu wa maadili, upweke, na jinsi mji unavyoweza kummeza mtu asiye na msingi imara.

ITAENDELEA TOLEO LIJALO….

NIDHAMU CHANYA

9.2 Utangulizi

Nidhamu ni sehemu muhimu katika malezi ya mtoto, kwani humsaidia kuelewa mipaka, wajibu, na tofauti kati ya mema na mabaya. Hata hivyo, nidhamu bora siyo ile inayotumia ukali au adhabu kali, bali ile inayojenga uelewa na kumfundisha mtoto kuwajibika kwa matendo yake. Nidhamu chanya inalenga kumlea mtoto kwa kutumia maelekezo, mazungumzo, na mifano bora ya tabia. Katika sehemu hii, tutachunguza umuhimu wa nidhamu chanya, faida zake, na jinsi inavyoweza kumsaidia mtoto kuwa na maadili mema na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika maisha yake ya sasa na baadae.

9.2.1 Nidhamu Chanya

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

Nidhamu chanya ni njia ya kumlea mtoto kwa kumfundisha tabia njema kwa kutumia upendo, maelekezo, na mwongozo badala ya ukali au adhabu kali. Mtoto anapolelewa kwa nidhamu chanya, hujifunza kuelewa matendo yake na matokeo yake, badala ya kuogopa adhabu. Kwa mfano, mzazi anapomueleza mtoto kosa lake na kumfundisha namna ya kulirekebisha, mtoto hujifunza kuwajibika na kufanya maamuzi sahihi. Nidhamu hii hujenga msingi wa mtoto kuwa na heshima, subira, na uwezo wa kujidhibiti katika maisha yake ya kila siku.

9.2.2 Faida Katika Nidhamu Chanya Katika Malezi

Faida za nidhamu chanya ni nyingi na zina mchango mkubwa katika ukuaji wa mtoto. Kwanza, humsaidia mtoto kujenga uwezo wa kujidhibiti. Kwa mfano, mtoto anapofundishwa kuelewa matokeo ya matendo yake badala ya kuogopa adhabu, hujifunza kufikiri kabla ya kufanya jambo. Pili, nidhamu chanya hujenga uhusiano mzuri kati ya mzazi na mtoto. Mtoto anapohisi kueleweka na kusikilizwa, huwa tayari kushirikiana na mzazi wake bila kulazimishwa. Tatu, humsaidia mtoto kujifunza kuwajibika kwa matendo yake. Mfano ni mtoto anayefundishwa kurekebisha kosa lake badala ya kuadhibiwa tu, hujifunza thamani ya uwajibikaji na heshima kwa wengine.

9.2.3 Hasara Za Kukosa Nidhamu Chanya Katika Malezi

Kukosa nidhamu chanya kunaweza kuleta changamoto nyingi katika malezi ya mtoto. Mtoto anayekuzwa kwa ukali au adhabu kali mara nyingi hujifunza kuogopa badala ya kuelewa. Hali hii inaweza kusababisha mtoto kuwa na hofu, kukosa kujiamini, au hata kuwa na tabia ya uasi. Kwa mfano, mtoto anayeadhibiwa bila kuelezwa kosa lake anaweza kurudia makosa yale yale kwa sababu hajajifunza sababu ya kuyakwepa. Aidha, ukosefu wa nidhamu sahihi unaweza kusababisha mtoto kushindwa kujidhibiti na kushindwa kuheshimu wengine, jambo linaloweza kuathiri maisha yake ya kijamii na kielimu. Ko

9.2.4 Nini cha Kuzingatia Katika Nidhamu Chanya

Ili nidhamu chanya iwe na mafanikio, mzazi anapaswa kuzingatia mambo kadhaa muhimu. Kwanza, kutoa maelekezo kwa upole na uwazi, ili mtoto aelewe kile kinachotarajiwa kwake. Pili, kuwa thabiti katika maamuzi na kanuni za familia, ili mtoto asichanganyikiwe na ujumbe tofauti. Tatu, kuzingatia umri na uwezo wa mtoto, kwani kila hatua ya ukuaji ina mahitaji yake. Pia, mzazi anapaswa kuwa mfano mzuri

wa tabia, kwani watoto hujifunza zaidi kwa kuona kuliko kusikia.

9.2.5 Njia za Kuimarisha Nidhamu Chanya Katika Malezi

Kuna njia mbalimbali za kuimarisha nidhamu chanya katika malezi ya kila siku. Kwanza, kutumia mazungumzo badala ya adhabu kali, kwa kumweleza mtoto kosa lake na jinsi ya kulirekebisha. Pili, kutoa pongezi na kutambua tabia nzuri, ili kumtia moyo mtoto kuendelea kufanya vizuri. Tatu, kuweka mipaka iliyo wazi na kueleweka, ili mtoto ajue kile kinachoruhusiwa na kisichoruhusiwa. Pia, mzazi anapaswa kuwa na subira na kutoa mwongozo kwa upendo, kwani mabadiliko ya tabia huchukua muda.

9.2.6 Vikwazo Vinavyoweza Kuzuia Nidhamu Chanya Katika Malezi

Katika mazingira ya sasa, kuna vikwazo vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa nidhamu chanya. Moja ya changamoto ni msongo wa maisha unaowafanya wazazi kukosa muda au subira ya kuzungumza na watoto wao, na hivyo kuishia kutumia adhabu kali. Pia, ushawishi wa teknolojia unaweza kuathiri nidhamu, kwani watoto wanaweza kujifunza tabia zisizofaa kutoka mitandaoni bila uangalizi wa wazazi. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa msimamo mmoja kati ya wazazi au walezi, jambo linaloweza kumchanganya mtoto kuhusu kile kinachotarajiwa kwake.

Hitimisho;

Nidhamu chanya ni msingi muhimu katika malezi bora ya mtoto. Bila nidhamu inayojenga uelewa na uwajibikaji, mtoto anaweza kukosa mwelekeo sahihi wa tabia na maamuzi. Kwa kutumia njia za upendo, maelekezo, na mfano bora, mzazi au mlezi humsaidia mtoto kukua akiwa na uwezo wa kujidhibiti, kuheshimu wengine, na kufanya maamuzi sahihi katika maisha yake. Nidhamu hii humjenga mtoto kuwa mtu mwenye maadili, subira, na uwajibikaji, jambo linalomuwezesha kuwa raia mwema katika jamii na familia yake.

Abbas Mahmoud Al-Aqqad

Inatoka ukurasa wa 18

Upana huu ulionekana wazi katika maandishi yake yaliyochanganya kina cha fikra na uzuri wa lugha ya kifasihi, yakawa muunganiko wa mantiki na ubunifu, uchambuzi na umakini.

Katika uwanja wa ushairi, Al-Aqqad alikuwa mmoja wa waanzilishi wa mageuzi, akijaribu kuikomboa mashairi kutoka katika mipaka yake ya jadi na kuyaunganisha zaidi na maisha na mwanadamu. Alitoa diwani kumi za mashairi, zilizowakilisha muhtasari wa uzoefu wake wa zaidi ya miaka hamsini, akieleza mtazamo wake kuhusu dunia na tafakuri zake kuhusu maisha na mwanadamu.

Al-Aqqad alipata heshima kubwa katika maisha yake, akachaguliwa kuwa mwanachama wa Academy of the Arabic Language in Cairo, na akatunukiwa Tuzo ya Taifa ya Fasihi. Wataalamu wakubwa wa fasihi walimsifu, hususan Taha Hussein, aliyemwona kuwa anastahili kuongoza ushairi wa Kiarabu baada ya Ahmed Shawqi na Hafez Ibrahim. Heshima hii haikuwa isipokuwa ni kielelezo cha nafasi yake ya kweli, aliyojijengea kwa juhudi na akili, si kwa mamlaka au hadhi.

Al-Aqqad aliendelea kuwa mwaminifu kwa kalamu yake hadi mwisho wa maisha yake, hakuacha kuandika wala kuchoka kutafiti, hadi alipofariki dunia mwaka 1964 baada ya maisha yaliyojaa juhudi, kazi na ubunifu. Aliacha nyuma urithi mkubwa wa kielimu na kifasihi ambao bado unaishi ndani ya utamaduni wa Kiarabu, ukiwa ushahidi kwamba nia thabiti na akili iliyoangaziwa vinaweza kujenga utukufu, hata katika mazingira magumu.

K.O.K.W.A—3

Ilipoishia…
"Makosa ambayo yatagharimu uhai wangu… hata hivyo ni kwa ajili yako," akaongea kwa sauti ya chini lakini ilikuwa 'stereo' kwelikweli.
"Wewe ni nani?" Amata akarudia swali, "Na kwanini uweke maisha yako reheni kwa ajili yangu?" akaongeza swali. Akatazama saa yake, ilitimu saa moja na dakika kumi na mbili jioni. *Bado dakika tatu windo langu lifike!* Akawaza.

Endelea…

Akarudisha macho kwa yule mwanamke.
"Naitwa Afrika!" yule mwanamke akajibu.
"Afrika?" Amata akauliza ili kupata uhakika.
"Ndiyo, najua itakushangaza, ila jina langu ni Afrika…" akajibu tena. Amata akaona mwanamke yule anampotezea muda. Ametumwa! Akawaza. Uwepo wangu ushajulikana hapa, sasa nione la kufanya kwa muda! Akajiambia moyoni mwake.

"Asante Afrika, kwaheri… sipo kwa huduma unayotaka kunipa. Ila nikimaliza kazi yangu nitakutafuta unihudumie," Amata akasema huku akianza kuuelekea mlango.
"Sivyo Amata! Hivi we ni mpelelezi gani ambaye hata ushangai nalijua jina lako kwa ufasaha namna hii?" Afrika akauliza.
"Kwa kazi yangu, kila mtu analijua jina langu, tena analijua zaidi ya mimi ninavyolijua… sishangai!" ASmata akasjibu na kushika kitasa.
"Sikiliza Amata! Wanajua kama upo Antatanarivo, wanajua nyendo zako zote, wanajua kama saa hii utakuwa eneo hili, wanajua kama unamtaka Mikhail Planchkov, wanajua kuwa umetumwa kuitafuta 'kokwa'…" Afrika alizungumza huku macho yake yakiwa yamejawa machozi. Amata aliondoa mkono kwenye kile kitasa na kusimama kidete. Akashusha pumzi na kumwangalia Afrika pale alipoketi. Afrika



aliinua mkono wake na kuuelekeza kichwani pake ili kutoa ua alilojipamba. Macho ya Amata yalikuwa yakiufuata mkono huo na yalipotua, moja kwa moja yalikuwa yakitazama dirisha lile kubwa. Lahaula! Macho yake yalijikuta yakitazamana na bomba la bunduki ya kirussia likimtazama. Kwa harakaharaka aliijua bunduki hiyo, IZMASH Saiga12 gauge. Akili ya haraka ikamjia. Tunashambuliwa! Akawaza na kujirusha upande wa pili. Kioo cha lile dirisha kikatawanyika vipande vipande na kuleta tafrani ndani ya kile chumba. Risasi zile tatu zilizomkoa Amata ziliishia ukutani. Akachomoa

bastola yake na kusimama nyuma ya pazia akitupa jicho huku na huko. Amata akawahi kwenye dirisha jingine na kuvuta pazia kuangalia nje. Aliona vijana wawili wa Kiafrika wakitoka kwa kukimbia kwenye ile hoteli. Vijana wale walikuwa wakielekea kwenye jengo lilelile alilokuwamo yeye na Afrika.

Kisha Mzungu mmoja mtu mzima akatoka kwenye mlango mkubwa wa ileile hoteli akisindikizwa na watu wegine wawili wakaingia kwenye gari na kuondoka kwa kasi. Amata akashusha paumzi na kuuelekea ule mlango. Akafungua na kuuacha wazi kidogo. Haikupita dakika akahisi mlango mkubwa wa sebuleni ukifunguliwa. Muda wote huo, Afrika alikuwa sakafuni kimya. Damu kidogo ilionekana kwenye kifua chake. Amata akatulia palepale ili kuona kitachojiri. Hakukosea, domo la IZMASH Saiga likatangulia huku likiusukuma mlango taratibu. Amata akatulia kimya na kusubiri sekunde kadhaa alizozitaka.

Yule bwana akaonekana kusimama mlangoni, maana domo la ile bunduki halikusogea kuingia ndani. Kwa kasi ya ajabu, Amata alikamata ule mtutu wa IZMASH Saiga na kuvutia ndani. Yule jamaa akajikuta kaingia pasi na kutarajia. Pigo moja lililopigwa kwa umahiri lilitua nyuma ya shingo ya huyo bwana. Akapepesuka na kuvuta hatua za kiwewe mbele. Kabla hajatulia alijikuta anapigwa kabali ya shingo na kuvutwa chini. Akabwagika kama gunia la mpunga. Risasi moja ikadidimia mwilini mwake. Amata alipomnasua kwenye ile kabali, yule jamaa alitepeta.

"Wewe ni nani?" akamuuliza. Yule bwana alikuwa akivuta pumzi zake za mwisho-mwisho. Hakujibu, aligeuza sura na kumwangalia Amata huku povu likimtoka kinywani. Kwa haraka Amata akampekuwa kijana yule. Akachukua kitambulisho chake, leseni ya kuendeshea gari, simu ya mkononi. Kishindo cha mlango kupigwa kwa nguvu kikamgutusha pale chini. Kamanda Amata aliruka sarakasi na kutoka kwenye lile dirisha kubwa mpaka nje ambapo alianguakia juu ya jengo fupi jingine. Risasi kadhaa zilimkosa. Maumivu ya mgongo yalimtambaa mwili mzima lakini hakuwa na muda wa kuyatii. Alivingirika na kujirusha chini ambapo alitua juu ya vyakula vilivyokuwa vikiuzwa hapo barabarani. Alichojua ni kunyanyuka na kutimua mbio kutafuta usalama wake huku watu wakipiga kelele za kumshangilia wasijue nini kimetukia.

Kamanda Amata aliegesha gari lake nje ya hoteli ya Le Combava. Akateremka na kuelekea chumbani kwake. Alipoufikia mlango akasimama kwanza kabla ya kufanya lolote. Akatazama baadhi ya alama zake alizoweka na kuzikuta zipo salama kabisa. Hawajaja! Akajiambia na kupachika kadi ya kufungulia mlango. Ni kwa kupachika kadi hii tu ndipo utaruhusu kila kitu kifanye kazi ndani ya chumba hicho. Alitoa kila kitu alichohukua kwa yule jamaa na kubwaga kitandani. Akaliendea begi lake na kutoa vidonge kadhaa akameza ili mwili wake utulie dhidi ya maumivu makali. Akavua nguo zote na kujinyoosha kidogo.

Alipoona mwili upo sawa kwa kiwango fulani akaliendea bafu ili ajimwagie maji. Alipopiga tu hatua kuingia bafuni humo, almanusura aanguke. Alichokiona kwenye beseni kubwa la kuogea hakikuwa kitu cha kawaida.

Mwili mbichi wa Afrika ulikuwa umelazwa ndani yake huku shingo ikining'inia upande wa pili na kuacha koromeo linalovuja damu nzito. Amata alihisi kama kapigwa shoku ya umeme, aliganda akiwa katoa macho. *Wamemleta saa ngapi hapa?* Akajiuliza.

Soma riwaya hii kupitia

www.kitabumarket.co.tz

RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (10)- Na: Eva Mrema

Ilipoishia…

Nililia mithili ya mama aliyefisha mwana. Sunche alikuja mbele yangu na kupiga goti, hakujali kabisa wapitaji waliofuata huduma pale hospitali. Alinyoosha mikono yake miwili na viganja vyake vikubwa vikalikumbata tumbo langu.

Endelea…

Ukimya wa sekunde chache ni kama aliutumia kukusanya nguvu.

"Nitakuwa baba! Nitakuwa baba jamani! Uuuhh! Nitakuwa baba mimi Sunche!" Aliyasema haya kwa ukelele kiasi kwamba watu walioletwa pale na shughuli zao za kimatibabu walijikuta wakituzingatia sisi.

"Tafadhali kaka tuko eneo la hositali, usirudie kupiga kelele" mlinzi alimweleza Sunche.

Sunche alinyanyuka na kumkaribia, "ukiambiwa utakuwa baba wakati una zaidi ya miaka arobaini utafanya nini?" Sunche alimuuliza mlinzi ambaye alisisitiza matumizi ya sauti ndogo eneo la hospitali.

"Eti waungwana, ukiambiwa utakuwa baba na mwanamke unayempenda kama nafsi yako mwenyewe utafanya nini? Furahia kaka, tunaishi mara moja" Sunche alionekana kama mtu aliyepagawa kwa furaha. Alimnyanyua mlinzi wa hospitali juu na kumshusha mara moja. Alinirudia, alinikumbatia na kunipiga mabusu kedekede. Tabasamu liliniwamba usoni. Kama mwanamke kuna namna nilihisi soni juu ya macho ya watu yaliyokodoka kisawasawa, ila nilimuacha asali wangu aufurahie ujumbe bora zaidi kuwahi kuupokea maishani mwake, kwa mujibu wa kauli zake mwenyewe.

Alinibeba na kunitua, alimkumbatia mdogo wangu. Baada ya kila mbwembwe iliyoashiria furaha tulikubaliana kuondoka. Nilipitia kadi yangu ya bima mapokezi, na kuwafuata mlangoni waliponingoja tutoke pamoja. Sunche alininyanyua juu kitu kilichofanya nicheke kama mwehu. Mdogo wangu alikomaa na picha mnato na picha mjongeo kama vile aliahidiwa donge nono kama malipo ya kuwa mtunzaji bora wa kumbukumbu za kufurahisha.

Nilibebwa hadi eneo lilipo gari. Aliniweka chini na kufungua mlango wa gari. Nilipanda kwa msaada wake naye akafunga mlango. Dogo na Sunche wakaingia garini na kila mmoja kuchukua nafasi yake. Mara hii tuliketi nyuma na mdogo wangu aliendesha.

"Tafuta hoteli nzuri tukasherehekee tafadhali, Arusha tutakwenda kesho" Sunche alimwambia shemeji yake.

"Mpenzi, likizo yangu inaisha rasmi kesho, nilitamani kufika mapema ili nifanye maandalizi, nipate na muda wa kupumzika" nilimwambia Sunche.

"Kwanini nipo? Nitakuandalia kila kitu na wewe utapumzika, naomba tufurahie siku ya leo kipenzi" baada ya Sunche kuongea, kauli naitoa wapi mimi? Nilitii, na safari ikaendelea. Tulirudi njia ya kuelekea Moshi ya zamani. Tuliulizia na kuelekezwa Rose garden. Paliwika sana kwa mazuri yote ya kiburudani.

Tulikula vizuri, tulikunywa kwa furaha na jioni tulitoka na kutafuta hoteli ya kulala. Tulipata. Palikuwa pazuri sana, tuliingia vyumbani na kupata japo wasaa wa kukogesha miili yetu baada ya siku ndefu. Tobiasi alikwenda chumbani kwake na simu yangu. Alifanya zoezi la kunyonya data na kuziweka kwenye tarakilishi, kisha alitunza kwenye kikasha cha kuhifadhia ndani ya barua pepe yangu. Mdogo wangu alikuwa kama kaimu wangu wa kujitolea. Vitu vingi kanifundisha yeye haswa vya kimtandao. Hapo awali sikujua chochote juu ya kutunza kumbukumbu kidigitali, sasa kila jambo muhimu nisilotaka kulipoteza nililitunza kwenye barua pepe yangu.

RIWAYA: NGUVU YA KIAPO

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

KITABU - Tsh 10,000
Dar es salaam:

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

Kwakuwa yeye ndiye alinifungulia basi nywila zote anazijua. Mimi na hani wangu kila dakika ni sikukuu, yaani tukitazamana tu, pilau linalika. Tulifanya yetu na mwisho tulijimwagia maji na kujiweka sawa. Sunche aliniaga kuwa kuna jambo anataka kushughulikia mimi nipumzike. Na hivi alinipa dozi murua dakika chache zilizopita, sikuwa na ubishi, nililala kabla hajamaliza hata kufunga mlango.

Usingizi wa zaidi ya saa tatu, tena za jioni uliniweka kwenye nafasi ngumu sana, niliota ndoto ambayo sikuikumbuka hata nukta. Kwa hakika ilitisha na kuniachia ujumbe wa hofu na mashaka moyoni; kumbukumbu za matukio zilitoweka. Nilimuita Sunche ila hakuitika. Giza lilitamalaki sikujua kama tayari ilitimu saa tatu usiku. Niliogopa vibaya mno, nilihisi mchakacho wa mlango kufunguliwa nilianza kutokwa na machozi. Nilihisi kabisa nimevamiwa. Niliita Sunche bado hakukuwa na tumaini la kuitikiwa. Mlango ulimtii mfunguaji, ukafunguka, nilishika shuka na kujifunika gubigubi. Nilisali sala zangu zote hadi zile za akiba. Nilisikia taa ikiwashwa.

Hapo natetemeka na kukazana kuomba nisidhuriwe. Nilihisi kuguswa juu ya shuka, hapo nilikunjamana nalo zaidi, "usinidhuru jamani nakusihi" niliongea kwa mashaka makuu.
"Dada, una shida gani wewe? Sauti ya mdogo wangu ilipenya masikioni na kunifanya nihangaike kujinasua ndani ya shuka nililojiviringishia kwa hiyari yangu. Nilipambana haraka haraka, nilipofanikiwa kutoa mikono na uso, dogo aliona hofu ilivyonishambulia bila huruma. Alinikaribia na kunikumbatia kwanza, bado niliweweseka. Aliniuliza kama nimevaa nguo, nikamjibu ndio, alifanya kazi ya kunitolea shuka lililoning'ang'ania kama vile nilizaliwa nalo. "Naogopa! Nilimwambia mdogo wangu.
"Uliota ndoto mbaya? Au unaogopa nini ccy?" Aliniuliza hali kanishika viganja vya mikono yangu.
"Hata sielewi, nimeshituka usingizini mwenye hofu na mashaka kedekede, bila shaka kuna ndoto nimeota mbaya ila siikumbuki" nilimjibu. Alinikumbatia na kunitaka niamke niusuuze uso kisha twende tukapate mlo wa jioni. Nilimuulizia mpenzi wangu, nikajibiwa kuwa aliningoja kwa hamu kubwa mgahawani.
Nilikurupuka kama mwehu, nilisuuza uso na kuswaki kinywa kwa sekunde zisizozidi hamsini. Niliingia msalani kupunguza maji kisha nikatoka.
"Twende" nikamwambia dogo.
"Dada, vaa japo kagauni, ka kitofauti basi, kweli mtaiti huo na shati nyeupe kama muuguzi wa zamu? Jiweke sawa kuna mzigo wako hapo mezani nakungoja nje" baada ya Tobiasi kusema hivyo akili ikaniwasha, nikatazama huku kisha kule kweli kifungashio nilikiona, kwakuwa sikukijua nilikiendea moja kwa moja. Nikakifungua kwa tahadhari kubwa. Nilikutana na nguo nzuri sana. Niliikunjua, ilikuwa gauni la rangi ya dhahabu, ndefu ya kushika mwili. Nilipoizingatia nilibaini kipande cha karatasi chini. Nilikinyanyua na kukisoma.

"I will be your costume designer tonight darling. Put on that dress, put on your black hills, wear earrings and a black necklace and then apply pink lipstick. Don't forget to use your American secret perfume. Welcome downstairs for dinner sweetie"

Ujumbe ulinifurahisha, nilivaa gauni ile ya rangi ya dhahabu, nilivaa viatu virefu vyeusi sambamba na mapambo meusi; yaani mkufu, hereni bangili na kibanio cha nywele. Nilipaka wanja na rangi ya mdomo ya pinki. Sikupaka poda tayari ni usiku na kwa namna fulani ngozi yangu inajitosheleza. Nilionekana maalumu sana. Nilitoka nje na kumkuta dogo, alinitazama na kunitazama tena.
"Umependeza sana ccy. Yaani namaanisha umewaka vibaya mno, hebu nishike mkono twende" nilitabasamu tu, aligeuka na kuufunga mlango kwa kadi kisha tukaondoka. Tulikuwa ghorofa ya ishirini na mbili. Tuliingia kwenye *'lift'* na dogo akabonyeza namba iliyomaanisha tunaelekea ghorofa ya nne. Tulitumia takribani dakika tano kufika tulikotakiwa. Alitoa kitambaa na kunifunga machoni. Alinishika mkono na kuniongoza, niliuliza maswali mengi na jibu lilikuwa moja tu, "vumilia kidogo".

KUMRADHI

Katika toleo namba 51, tulichapisha kwa kukosea herufi za jina la mwandishi A.E Musiba.

Tunaomba, badala ya kusomeka Elvis Elistabulus Musiba, sasa isomeke Aristablus Elvis Musiba. Tunawaomba radhi kwa usumbufu.

KALAMU YANGU

USIKU WA DENI—Na Gwamaka Mwamasage

USIKU WA DENI ni moja ya riwaya zinazotamba sana hapa nchini kwa sasa. Riwaya hii iliyoandikwa na Gwamaka Mwamasage inaagazia swalazima la ufisadi na ulaghai wa kimapenzi.
Ngurumo ya Mwandishi safari hii nikiwa na KALAMU YANGU tumstafuta mwandishi huyu namwishowe tumempata huko Mtwara...

Ulifikiri Nini au Nini kilikusukuma kuandika Riwaya ya USIKU WA DENI?

Huwezi kuamini, wazo la hii riwaya halikuwa hili lililotokea. Mimi ni aina ya waandishi ambao wazo linaweza kubadilika wakati wowote kadri ninavyoandika. Naweza kujua mwanzo nisijue mwisho utakuwaje ama kisa kinaweza kuwa cha namna fulani lakini kadri ninavyoandika kinabadilika. Kwa hiyo, nilichofikiri wakati ninapanga kuandika riwaya ya USIKU WA DENI sicho kilichotokea mwishowe.

Ok... Sasa je wahusika wako uliowatumia kwenye USIKU WA DENI hii ambayo tumeisoma, ndiyo haohao ambao uliwafikiri mwanzo?

Hapana, ilibidi wabadilike kulingana na muktadha

Mhusika yupi ambaye hata wewe mwenye unamkubali?

Binafsi namkubali Dah Ruh kwa namna alivyoweza ku-potray namna watu walivyo na pesa mjini zisizo na maelezo, namna ambavyo watu wanawekwa mjini na vibopa na namna ambavyo alitumika na kamati ya ulinzi na usalama kuvuruga siasa za Zahoro. Hapa nilijaribu kueleza vile kuna vitu vinaweza kutokea vikiwa vimepangiliwa kimedani bila kueleweka.

Tupe mrejesho kutoka Kwa wasomaji, je nao wamekongwa na Dah Ruh au Kuna mwingine?

Wengi wamekoshwa na Ngoma Kizito, mlinzi wa Mgombea aliyepotea katika mazingira ya kutatanisha hali iliyopelekea chama cha upinzani kupata ajenda.

Tuambie, je Kuna kisa Cha kweli kilichokusukuma kuandika Riwaya hii?

Kwa kuwa riwaya zangu nyingi zinapoteza mwelekeo kadri ninavyoandika huwa sio rahisi kuibua kisa cha kweli katika simulizi. Kwa

GWAMAKA MWAMASAGE
mwandishi wa kitabu
USIKU WA DENI



hivyo, USIKU WA DENI ni riwaya bunifu ikiundwa na visa vidogo vidogo.

Lakini, msanii ni mtabiri kulingana na mwenendo wa kijamii. Wakati nikiandika sikuwa nimeshuhudia kisa chochote, lakini leo wale waliosoma riwaya hiyo hunirudia na kuniuliza nilijuaje haya yangetokea?

Tukiendelea kukitazama kitabu hiki, unafikiri kinawezaje kumjenga msomaji kuwa Mtaznania bora?

Kitabu cha USIKU WA DENI kinaweza kumjenga Mtanzania kulingana na dhamira zilizoibuliwa ndani yake ikiwemo mapenzi, ndoa, siasa na upelelezi.

Lakini pia, kinajenga Mtanzania anayeweza kujenga udadisi juu ya masuala kadha wa kadha yasiyo na majibu ya moja kwa moja.

Kwanini ulichagua anwani USIKU WA DENI?

USIKU WA DENI ni anwani iliyojengwa a nkasahuu. Ambapo tama ya madaraka ya mhusika aitwaye Zahoro Panjinga iligeuka deni juu ya mipango yake, lakini mambo yalipokwenda kombo, alijikuta nafsi yake ikiingia deni la dhamiri ili kumthibitishia mkewe usahihi wake, hata hivyo aliishia kuangukia pua.

Je kitabu hiki kwa ujumla wake kinaeleza maana ya methali Usiku wa deni…?

NDIO au HAPANA.

Kama msomaji bado hujapata kusoma kitabu hiki cha Usiku wa Deni kilichoandikwa na Gwamaka Mwamasage, hujachelewa. Kinapatikana dukani kwetu Kona ya Riwaya, Kinondoni, tupigie simu 0655428085

DINA TULI
rest in peace

KILA mtu alipigwa na bumbuwazi, hakuna aliyeamini, kwani tanzia ya Tuli ilitufika tukiwa tunasubiri 'episode' inayofuata ya hadithi tamu aliyoitambulisha kwetu kwa jina ……

Sikuwa namfahamu vizuri binti huyu, mwandishi katika mitandao ya kijamii. Nachelea kusema kuwa maoni yawatu mbalimbali waliokuwa karibu naye, au tuite waliokuwa hadhira yake yalinishtua. Hapo sasa ndipo ikabidi nifuatilie kujua 'ni nani huyu?'

Katika kutafuta habari yenye uhakika hatimaye tulitaarifiwa kuwa Dina Tuli alifariki mnamo Mei 1 2026 majira ya saa 10 jioni. Taarifa hiyo ilisema kuwa Dina Tuli hakuugua na wala hakuwa na dalili ya ugonjwa wowote. Ni homa tu iliyomkuta jioni hiyo na kukimbizwa Hospitali ya Alexia ambako mauti yalimkta. Dina Tuli alizikwa tarehe 2 ya mwezi Mei. Marehemu ameacha watoto pacha wa miaka mitatu. Mungu amrehemu moendwa wetu.

Posti yake ya mwisokabisa kwenye mtandao wa Facebook aliituma tarehe 1 ya mwezi Mei siku hiyohiyo ambayo aliiaga dunia. Ilisomeka…

Umeme umetukatili ila tutaendelea na usaliti 03

Posti hii ilipata hoja takribani 510 lakini nyingi yazo zilimuomboleza. Hakuna aliyeamini kama mwandishi huyu wa hadithi kama Usaliti wa Kaka, Mapacha, na nyinginezo kwenye mtandao maarufu wa Facebook ametutoka.

Nini kingine cha kusema? Dina Tuli tutakumiss sana… endelea kupumzikakwa amani peponi…

Tangazo

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi
kila baada ya miezi miwili
jamvilasimulizi@gmail.com